epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Machi 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581612
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**KANE HATAKI MCHEZO BUNDESLIGA**

UKURASA 22

MIAKA 3 YA SAMIA

**Sekta** za uvuvi, mifugo zainuliwa; uhaba wa chakula si kilio tena nchini



UKURASA 3

**Kesi** ya msanii Marioo madai ya milioni 500/- kunguruma



UKURASA 5

**Mkakati** wasukwa kuongeza thamani mwani Zanzibar

UKURASA 17

# Unyanyapaa majaji na mahakimu tishio

• **Wengi** wakumbwa na msongo wa mawazo, Jaji Mkuu afichua kilichomo ndani ya mtungi...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### IDADI WANAFUNZI WANAOLAWITIANA NA KUBAKANA SHULENI YAONGEZEKA

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limesema kuna ongezeko la vitendo vya ubakaji na ulawiti vinavyohusisha...

UKURASA WA 21

### VINICIUS JR ANATENDWA VIBAYA - ANCELOTTI




KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema Vinicius Junior anatendewa vibaya zaidi uwanjani kuliko...

## Aibu mtaani chanzo mama kuua wanawe kwa soda yenye sumu

UKURASA 5





Wanawake wakiwa ndani ya magari ya kuongoza watalii kuelekea Hiifadhi ya Nyerere. **Picha ndogo;** Judith Ligenzi (katikati) akiwaelezea abiria wake jinsi anavyofanyakazi yake ya kuendesha treni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KINAMAMA 300 HIFADHINI

## Dereva wa treni mama, hakuna anayejutia safari hiyo

UKURASA 4

**MICHEZO** **GAMONDI ATAJA UGUMU WA IHEFU** UK.24 **KABWELA** UK.7



Wafanyakazi Wanawake wa mgodi wa Barrick North Mara wakiwa katika picha na watoto wanaolelewa katika kituo cha City of Hope kilichopo wilayani Tarime na kukabidhi msaada wa vitu mbalimbali katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Unyanyapaa majaji, mahakimu tishio

**Na Maria Seme**

MAJAJI na mahakimu wanyanyapaliwa na jamii kutokana na hukumu wanazotoa mahakamani, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, amesema.

Akiwa na angalizo mahususi kwa watendaji wenzake wa mahakama, Jaji Mkuu Juma ameanika vitendo vya unyanyapaa kwa kundi hilo, akiwataka majaji na mahakimu wanawake kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi kwa kuwa wao ndiyo kundi linaloathiriwa zaidi na unyanyapaa huo.

Amesema kufanya mazoezi na kupuuza mashambulizi dhidi yao kwenye mitandao ya kijamii kunaepusha msongo wa mawazo unaowakuta wanapofanya uamuzi kwenye kesi mbalimbali.

Akizungumza katika kongamano la kusheherekea Siku ya Kimataifa ya Majaji na Mahakimu Wanawake jijini Dar es Salaam jana, Prof. Juma alitoa mfano wa yaliyomkuta kwa watu aliowakuta mahali kumkimbia, lakini hakuchukulia maanani na kutoathirika kisaikolojia.

"Hivyo, majaji na mahakimu wanapaswa kuzingatia hilo (kutotilia maanani unyanyapaa) na kufanya mazoezi mara kwa mara," alisema.

Akirejelea utafiti uliofanyika Marekani kuhusu msongo wa mawazo na ustahimilivu kwa majaji wa Marekani, Prof. Juma aliwataka watendaji wenzake wa mahakama kupambana na kikwazo hicho ili kufanya kazi zao vizuri.

Katika kongamano hilo ambalo pamoja na mambo mengine lilikuwa linaangazia tafakuri ya msongo wa mawazo kwa majaji na mahakimu wanawake, Jaji Mkuu alisema kuwa kwa mujibu wa utafiti huo wa Marekani, vipo visababishi 37 vya msongo wa mawazo kwa majaji na mahakimu, vikijumuisha mashambulizi katika mitandao ya kijamii.

"Kuna jaji mmoja mwanamke, siku moja nilimwuliza 'huwa ninaona unashambuliwa sana kwenye mitandao ya kijamii, unajisikiaje?' Nilitaka kujua anahimili namna gani kwa sababu wakati mwingine wewe unafanya kazi yako kwa kufuata haki, lakini yaliyoandikwa katika mitandao ya kijamii yanakukatisha tamaa.

"Sisi wengine tuliishazoea usipoandikwa wiki nzima kusemwa vibaya, huwa hatujisikii vizuri kwa sababu nimeshazoea ubishi na kushambuliwa, wakati mwingine nilitaka kutayarisha mito ya kulalia iliyoandikwa Ibrahim Hamis Juma ili wale wanaonishambulia wawe wakilala usiku, wanataja Ibrahim Hamis Juma.

Ni njia moja ya mbinu za kupambana na msongo wa mawazo," alisema.

Jaji Mkuu alitaja visababishi vingine ni matokeo ya uamuzi unaotolewa katika kesi mahakamani, akifafanua kuwa katika kesi wakati mwingine mwenendo wa ushahidi unaotolewa hauridhishi, lakini hakimu hulazimika kutoa hukumu kutokana na ushahidi uliotelwa, jambo ambalo hupelekea msongo wa mawazo.

Pia alisema wapo watu wanaofungua kesi mahakamani wakiwa ni ndugu wa familia moja, lakini hutaka jaji au hakimu kukaa upande mmoja na asipofanya hivyo humtaka jaji au hakimu huyo kujitoa katika kesi, jambo ambalo mara nyingi humwathiri kisaikolojia baada ya kuona kuwa wanaoleta kesi wanamtaka kupindisha sheria na kusimama na kundi mojawapo.

"Sababu nyingine iliyotajwa inasababisha msongo wa mawazo kwa majaji ni aina ya migogoro wanayoletewa. Unaweza kukuta wadaawa ni wa familia moja, wanapambana na migogoro yao ya nyumbani, wanaileta mahakamani na wanataka wewe jaji uegemee upande mmoja au mwingine na ukijaribu kuwa katikati unazua uadui.

"Wakati mwingine unaambiwa 'Mheshimiwa Jaji jitoe!' Unapojitoa wakati wewe unajua unataka haki na upo sahihi, hili vilevile husababisha msongo wa mawazo na wengine hubeba huo msongo na kwenda nao nyumbani," alifafanua Prof. Juma.

Mwenyekiti wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA), Jaji wa Mahakama ya Rufani, Barke Sehel alisema kuna ongezeko kubwa la majaji, mahakimu na watendaji wengine wa mahakama wanawake tangu mwaka 1970 ambapo Jaji mstaafu Eusebia Munuo kwa mara ya kwanza aliingia katika mfumo wa mahakama nchini akiwa ni mwanamke pekee.

Alibainisha kuwa kwa sasa katika Mahakama ya Rufani kuna majaji wanawake 13 kati ya 35 waliopo huku katika Mahakama Kuu kuna majaji wanawake 38 kati ya 105 waliopo.

"Jaji Eusebia Munuo ndiyo mwanamke wa kwanza kabisa kuingia katika mahakama zetu, aliteuliwa kuwa hakimu mkazi wa kwanza mwanamke mwaka 1970 na wakati ule hapakuwa na mwanamke yeyote aliyekuwa na nafasi katika mahakama zaidi yake, yeye peke yake nchi nzima.

"Pia alikuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya juu kabisa katika mahakama zetu mwaka 2002 alipoteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

"Mwaka ule alipoteuliwa kulikuwa na jumla ya majaji tisa wa Mahakama ya Rufani, ndiye alikuwa mwanamke peke yake na pia ndiye mwanzilishi wa TAWJA, alipata shida kukianzisha kwa sababu Chama cha Majaji Wanawake Duniani kilitaka pawapo angalau majaji 10, hawakufikisha idadi, ikabidi waombe wachanganye na mahakimu ndipo wakakubaliwa," alisema.

# Idadi wanafunzi wanaolawitiana na kubakana shuleni yaongezeka

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limesema kuna ongezeko la vitendo vya ubakaji na ulawiti vinavyohusisha wanafunzi wenye umri chini ya miaka 18 wanaotendana ukatili huo wanapokuwa shuleni.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama alibainisha hayo mjini hapa jana alipochangia mada kuhusu vitendo vya ubakaji na ulawiti vinavyoongezeka mkoani humu wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Morogoro (RCC ).

Alisema matukio ya vitendo vya ubakaji na ulawiti yanaongezeka kwa kasi mkoani Morogoro, waathirika wakubwa wakiwa ni watoto wakiwamo wanafunzi wenye umri wa kuitwa watoto

"Cha kusikitisha ni kuwa vitendo hivyo vingi watuhumiwa ni watoto chini ya umri wa miaka 18 kwa maana wenyewe kwa wenyewe wanafanyiana vitendo vya kulawitiana na kubakana," alisema.

Kamanda Mkama ambaye hakuweka wazi takwimu za ongezeko la vitendo hivyo, alisema matuko hayo mengi yanafanywa kwenye maeneo ya shule na yanafanywa na wanafunzi wenyewe kwa wenyewe.

"Katika uchunguzi wetu tumebaini hawa wanafunzi wanalawitiana zaidi ya mtoto mmoja au mtoto mmoja analawiti zaidi ya mtoto mmoja," alisema.

Kamanda Mkama alisema matukio hayo yamekuwa yanaongezeka siku hadi siku, hasa kipindi ambacho shule ndiyo kwanza zinakuwa zimefunguliwa; akiitaja miezi ya Januari, Februari na Machi kuwa kipindi hatari zaidi.

Alisema matukio hayo yanaongezeka nyakati hizo, yakiripotiwa kwao na waratibu elimu kata na madawati ya jinsia na watoto ya polisi.

Alisema athari za matukio hayo zinakuja kufahamika zaidi kuanzia miezi Januari hadi Machi, baadhi ya watoto wakibainika kuwa na ujauzito wanapopimwa afya zao.

Kamanda huyo alisema kuwa katika kipindi cha Novemba na Desemba, matukio hayo yanakuwa machache kutokana na wanafunzi kuwa likizo, wanakuwa chini ya uangalizi wa wazazi wao.

Kutatua tatizo hilo, Kamanda Mkama alisema Jeshi la Polisi linashirikiana na wadau wengine kutoa elimu shuleni kupitia dawati la jinsia.

"Sababu kubwa ya matukio haya ni mila na desturi zinazokiuka maadili mazuri kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro. Shule zinapofungwa kunakuwa na vigodoro (ngoma za asili) vingi," alilalama.

Kamanda Mkama alisema wazazi kutokutoa ushirikiano kwa kwenda kutoa ushahidi mahakamani huku wakimalizana kifamilia na wahalifu ni sababu nyinyine ya kushamiri vitendo hivyo, hata kukwamisha jitihada za kumaliza matukio hayo.

Alisema polisi imeshapendekeza kuwa tukio ubakaji na ulawiti linapotokea, mara moja aliyefanyiwa kitendo hicho atoe shahidi mahakamani badala ya kusubiri muda mrefu kwa vile muda wa kusubiria unatoa mwanya kwa pande mbili hizo kumalizana.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima alisema amekuwa akipatiwa taarifa na Kamanda wa Polisi Mkoa kila siku kuhusu vitendo vya ubakaji wanawake na watoto pamoja na ulawiti. Vimeshamiri mkoani mwake.

Malima alisema kutokana na kuwapo mfululizo wa matukio ya ubakaji wanawake, watoto na ulawiti, mkoa umejipanga kudhibiti matukio hayo na kuyakomesha.

Mkuu wa Mkoa alipandekeza kuitishwa kikao maalum na kumwalika Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima na timu yake kushiriki na kujadiliana kuwa na mkakati wa pamoja wa kudhibiti ukatili huo shuleni kwa kuangalia upungufu wa kisheria na kuwa na mpango endelevu wa utoaji elimu kwa jamii.

Januari 2020, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu madhila ya watoto kulawitiana shuleni wilayani Mkuranga, mkoani Pwani. Ilithibitishwa na mamlaka za serikali kwamba vitendo hivyo haviko wilayani Mkuranga au Mkoa wa Pwani pekee, bali pia mikoani mingine nchini, vitendo hivyo vikitajwa kushamiri zaidi mikoa ya Tanga na Dar es Salaam.

Vilevile, Januari mwaka jana, gazeti hili pia liliripoti kuhusu wanafunzi kufundishwa kulawitiana wakiwa shuleni katika baadhi ya shule binfasi mkoani Kilimanjaro huku baadhi ya walimu mkoani humo wakinaswa na serikali wakipatiwa mafunzo ya vitendo vya 'kisheni'.

## KUELEKEA MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA

# Ameinua sekta ya uvuvi, kukabiliana mabadiliko tabianchi, uhaba wa chakula

**Na Vitus Audax**

KILIMO na uvuvi ni miongoni mwa sekta zinazogusa moja kwa moja maisha ya mwananchi na uchumi wa taifa.

Licha ya Rais Samia Suluhu Hassan kupokea nchi katika kipindi ambacho ulimwengu unakabiliwa na majanga matatu makubwa ambayo ni mabadiliko ya tabianchi, ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na vita ya Ukraine na Urusi, sasa anafanikiwa kufikisha miaka mitatu kwa kuyakabili majanga hayo na kudhibiti baa la njaa.

Katika sekta ya kilimo, Rais Samia Suluhu Hassan alipokea nchi wakati uzalishaji wa chakula ukiwa umeshuka kwa zaidi ya tani milioni 1.5 ikiwa ni tofauti ya zaidi ya tani milioni 18.6 kwa mwaka 2020/21 na zaidi ya tani milioni 17.1 kwa mwaka 2021/22.

Kutokana na mabadiliko hayo uzalishaji wa chakula ulishuka katika nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania kufikia mwaka wa fedha 2022/23 hali iliyosababisha kupanda kwa bei za vyakula nchini.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Rais Samia aliiagiza Wizara ya Kilimo kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) iesambaze tani 75,282.302 za chakula katika halmashauri 89 zenye upungufu na kuuzwa kwa bei kati ya Sh. 680 hadi 920 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya soko ya Sh. 1,200 hadi 1,500.

Kadhalika, aliweka mpango wa kuendelea kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi chakula kutoka tani 251,000 za sasa hadi tani 506,000, mpango wa kujenga miundombinu ya uhifadhi chakula kuongeza uwezo wa kuhifadhi kufikia tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030 na kuwa na uwezo wa kuhifadhi chakula cha kutumia kwa muda wa miezi sita. Pia zilinunuliwa tani 18,294.314 za chakula ambako kati ya hizo, 17,257.857 za mahindi na 1,036.457 za mtama sambamba na bakaa ya tani 141,575.902 zikiifanya NFRA kuhifadhi jumla ya tani 159,870.216 katika ghala zake.

Pamoja na makabiliano ya upungufu wa chakula nchini Rais Samia alitekeleza vipaumbele 13 katika sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuimarisha utafiti kwa kutengewa na kutumia Sh.bilioni 40.73 ikiwa ni pamoja na kuzalisha mbegu.

Alitoa ruzuku ya mbegu za alizeti, ngano na miche ya chikichi, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kutoa huduma ya upimaji wa afya ya udongo, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji, kuimarisha huduma za ugani na kuhamasisha kilimo cha ukanda kutokana na ikolojia za kilimo.

Vilevile, upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo unatajwa kuimarishwa, mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa kuanzisha mfuko wa maendeleo ya kilimo, miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo, kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja, kuanza kutoa ruzuku ya mbolea mwaka 2022/2023, kuimarisha kilimo anga na maendeleo ya ushirika.

Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji nchini, ikiwamo mabwawa ya kuvunia maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji ili kuhakikisha uzalishaji unaongezeka bila kujali ya hali ya mabadiliko ya tabianchi.

Kwa kipindi cha miaka hiyo mitatu Tanzania imefikia eneo linalomwagiliwa la hekta zaidi ya 727,280 sawa na asilimia 60.6 ya lengo la hekta milioni 1.2 ifikapo mwaka 2025 ambako vilevile ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliyopangwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 uliendelea.

Waziri Bashe alisema mikataba ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya umwagiliaji zaidi ya 48 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 234 ilisainiwa huku ikitarajiwa kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 95,005 na kufanya eneo linalomwagiliwa kuwa hekta 822,285.6 sawa na asilimia 68.5 ya lengo.

Alitaja miundombinu ya umwagiliaji inayendelea kutekelezwa ikiwamo mashamba ya mbegu ya Kilimo - Nzega hekta 400, Arusha hekta 200, Msimba hekta 200 na Tengeru hekta 10 ambapo wamekamilisha uchimbaji wa visima virefu sita sawa na asilimia 75 ya lengo la kuchimba visima vinane katika shamba la mbegu la Msimba.

Kadhalika, linatajwa ongezeko la uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 3,033 mwaka 2021/2022 hadi tani 3,175 mwaka 2022/2023.

Katika kuhakikisha wakulima wanapata mbolea serikali iliweka ruzuku na kuruhusu uingizwaji, uzalishaji na usambazaji wa tani 650,000 za mbolea kwa msimu wa kilimo 2022/2023 kupitia TFRA iliyosaidia upatikanaji wa mbolea kufikia tani 819,442 ikiwa ni asilimia 126 ya lengo.


Kiasi hicho kilitokana na tani 75,399 zilizozalishwa nchini, tani 617,079 zilizoagizwa nje ya nchi na tani 126,964 bakaa ya msimu wa mwaka 2021/2022. Hili ni ongezeko la asilimia 46 ikilinganishwa na msimu wa 2021/2022 ambapo upatikanaji wa mbolea ulikuwa tani 560,551.

Aidha, sekta ya uvuvi imekua kwa kuongezeka kwa idadi ya wavuvi wadogo zaidi ya 197,760 na kuchangia asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini.

Vilevile, vyombo vya uvuvi vimetajwa kuongezeka hadi kufikia 58,448 na kuwawezesha wavuvi kuvuna tani 426,555.46 za samaki zenye thamani ya Sh.ttrilioni 2.86.

Kwa Mujibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega sekta hiyo imeendelea kukukua kwa kasi ikiwa ni baada ya kuanza utekelezaji wa mpango kabambe wa kuikuza lengo likiwa ni kuinua mchango wake katika uchangiaji wa pato la Taifa hadi kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka wa fedha 2036/37 kutoka asilimia 1.8 mwaka wa fedha 2021/22.

Katika kuanza utekelezaji wa mpango huo Rais Samia aliruhusu mapendekezo ya wadau mbalimbali ili kuongeza ubunifu katika kufikia malengo kupitia mpango huo wa miaka 15 unaosaidia kulinda, kusimamia, kuhifadhina kutumia rasilimali hizo kwa njia endelevu ili kuchangia kikamilifu katika utoaji wa ajira.



Sekta hiyo imeongeza mchango wake katika pato la Taifa kufikia asilimia 2.5, imetoa ajira kwa wavuvi 197,763 na wakuzaji viumbe maji 34,057 ambako watanzania milioni 4.5 wanajishughulisha na shughuli zinazohusiana na uvuvi.

Rais Samia pia aliendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji katika uvuvi wa kibiashara na kuwezesha ongezeko la meli tisa zilizomba vibali vya kuvua kambamiti kati ya hizo, meli nne zimekidhi vigezo na kupewa leseni huku meli sita zilizopata vibali 2022 zikivua tani 57.59 za kambamiti zenye thamani ya Sh. 835.04. 137.

Kwa kipindi cha miaka mitatu soko la mazao ya uvuvi limetajwa kuimarika zaidi ndani na nje ya nchi na kufikia na 29,466.98 za mazao ya uvuvi yenye thamani ya Sh. bilioni 453.8 na idadi ya samaki hai wa mapambo 150,308 wenye thamani ya Sh. bilioni 1.82 waliuzwa nje ya nchi huku tani 6.24 za samaki za Sh.bilioni 0.22 zikiingizwa nchini.

Waziri Ulega alitaja ongezeko la miundombinu ya ukuzaji viumbe maji katika kipindi hicho kufikia mabwawa 32,878, vizimba 71 993, vitotoleshi 39 vya kuzalisha vifaranga na viwanda nane vya kutengeneza chakula cha samaki.

Katika kuongeza upatikanaji samaki nchini uzalishaji wa mazao mbalimbali ya ukuzaji viumbe maji umeendelea ambapo umefikia tani 33,525.46 na vifaranga vya samaki 35,967,180 ambapo kati ya hivyo, vifaranga 31,000 vilipandikizwa katika malambo mbalimbali nchini.

Katika uwezeshaji wavuvi, Rais Samia ameendelea kutekeleza mradi wa kuwakopesha wavuvi boti 160 za uvuvi za kisasa na zana zake kwa wavuvi 989, vizimba 222 kwa wanufaika 1,213, kutoa na uzalishaji wa zao la mwani ambapo mikopo hiyo inatolewa kwa masharti nafuu chini ya usimamizi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Aidha, hivi karibuni mwishoni mwa mwezi januari mwaka huu Rais Samia akiwa jijini Mwanza alionesha nia ya kuendelea kukuza sekta hiyo kwa kutaja mambo kumi yanayoendelea kufanywa na serikali katika kuhakikisha sekta hiyo inakuza mchango wake katika pato la Taifa.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi wa Wizara hiyo,kuweka miundombinu wezeshi ya kibiashara, kuweka chombo/wakala atakaye simamia na kuangalia maendeleo ya sekta hiyo,kuwatambua na kuwaweka kwenye kanzi data wavuvi wote,wafugaji wa rasilimali maji,wachakataji wa mazao ya samaki pamoja na wafanyabiashara lengo likiwa ni kurasimisha ajira zao.

Alitaja ujenzi wa bandari kubwa za uvuvi katika ukanda wa Afrika Mashariki ambazo pia zinaendelea kujengwa Kilwa Masoko-Lindi na Bagamoyo, ujenzi wa masoko saba ya mazao ya uvuvi na mialo mitatu,ujenzi wa mitambo ya kuhifadhia mazao ya samaki na mitambo ya kuzalisha barafu.

Pia mpango wa ununuzi wa meli za kisasa za uvuvi,ujenzi wa vituo vya kuendeleza ufugaji wa viumbe maji, mashamba darasa ya ufugaji samaki pamoja kuongeza bajeti katika wizara ya uvuvi na ufugaji itakayoenda sambamba na kutangaza uwekezaji wa sekta hiyo.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**JACKSON MATHAYO MASSAWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 365 APR - TOYOTA RAFFINE.** Yenye chassis namba **SX1000001710.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Control number: **9910840425629.**

MAKALA MAALUM

# KINAMAMA 300 HIFADHINI

# Dereva wa treni mama, hakuna anayejutia safari

Na Mwandishi Wetu

NI saa 12.45 asubuhi, Machi 9, 2024, unasikika mlio wa honi ya treni ya Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA), ikiashiria kuanza kwa safari ya kwenda Hifadhi ya Nyerere, iliyoandaliwa kwa ushirikiano na Mamlaka hiyo pamoja na Hifadhi ya Taifa (TANAPA).

Wanawake zaidi ya 300 wameripoti tangu saa 11 alfajiri kwenye stesheni ya kupandia treni hiyo, TAZARA jijini Dar es Salaam, wakitokea maeneo mbalimbali nchini, baada ya kuhamasika na matangazo yaliyokuwa yakisambazwa na TANAPA na TAZARA ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kufanya utalii wa ndani kwa kupanda treni hiyo kwenda kwenye hifadhi hiyo.

Dereva wa treni, Judith Ligenzi, ambaye amefanya kazi hiyo kwa muda wa miaka 11, anatangaza kupitia kipaza sauti chake kuwa sasa safari inaanza ya kuelekea kwenye hifadhi hiyo iliyopo Mkoa wa Pwani na vituo ambavyo itapita kikiwamo cha Mwakanga ambacho itasimama kwa muda kupishana na treni ya ROVUS Rail inayotoka nchini Afrika Kusini iliyobeba watalii waliotembelea hifadhi hiyo. Reli ya TAZARA ni maarufu kwasababu ni njia ya treni za kimataifa pia.

Sauti za furaha zinalipuka ndani ya treni kutoka kwa wanawake hao baada ya kusikika tangazo hilo huku honi ikiendelea kutoa mlio wa kuanza kwa safari hiyo.

Judith anasema amejisikia fahari sana na amefurahi kuwa dereva wa wanawake wenzake na kuona furaha halisi za wanawake wenzake.

"Ninachoomba wanawake wawekeze watoto wao kwenye elimu na wasichague kazi kwamba hii ni ya wanaume hainifai," anasema.

DJ Sweetlady alikonga nyoyo za wanawake wenzake kwa disco lililochezwa kwenye moja la behewa lililotengwa na kuwawezesha kuserebuka kuanzia mwanzo wa safari hadi mwisho.

Tiketi ya kwenda kwenye utalii huo kwa kichwa ilikuwa Sh. 200,000 ambayo ilijumuisha usafiri wa kwenda na kurudi, chakula, magari ya kuwatembeza kwenye mbuga na fulana maalumu zilizovaliwa siku hiyo.

Afisa Mwandamizi wa Uhifadhi Kanda ya Mashariki kutoka TANAPA, Apaikunda Mungure, amesema mwitikio wa wanawake waliojitokeza kutembelea hifadhi hiyo ni mkubwa.

"Lengo tulilojiwekea lilikuwa wanawake 400, lakini tunajivunia kwasababu tumekusanya wanawake zaidi ya 300. Tumeweza kukutanisha wanawake na kuwa kitu kimoja."

Mhifadhi huyo anasema katika jumuiko hilo kulikuwa na wanawake wa kada mbalimbali wakiwamo viongozi, viongozi wastaafu, waliowahi kuwa wake wa viongozi, wafayakazi, wafanyabishara, wajasiriamali na kuwakutanisha pamoja.

Anasema TANAPA inaamini kuwa utalii wa ndani unaongezeka na mipango yao ni kuandaa maeneo mengine ya kutembelea ya utalii katika hifadhi zake.

Apaikunda anasema wazo la kufanya utalii kwa kutumia treni lilitolewa na wenzao wa TAZARA ambalo walilikubali na kushirikiana nao.

TANAPA imeshawahi kufanya safari za utalii wa ndani kwenye hifadhi ya Sadani, iliyopo Bagamoyo, mkoani Pwani, lakini ilikuwa ikihusisha wapendanao kwa mujibu wa Apaikunda.

Kogumba Matimika (86), pamoja na umri wake kuwa mkubwa anasema alihamasika kujumuika na wanawake wenzake kufanya utalii huo ili aweze kuona vivutio mbalimbali vilivyomo kwenye hifadhi hiyo na kusifu juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, za kutangaza kampeni ya utalii katika hifadhi zilizoko nchini.

"Imenihamasisha kwa sababu utalii hata sisi tunaweza kuufanya badala ya kuwaachia wageni, Rais Samia amesaidia sana kuutangaza utalii hii itahamasisha Watanzania wengi kujitokeza kufanya utalii wa ndani."

Kogumba, anasema pamoja na kufanya utalii, lakini imemuwezesha kukutana na wanawake wenzake na vile vile kupanua mawazo yake na kusaidia kuondoa msongo wa mawazo kwa wanaopitia tatizo hilo.

Halima Mamuya, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), ndiye aliyekuwa mgeni rasmi katika safari hiyo kwa kukata keki rasmi hifadhini baada ya kufanya utalii wa kuangalia wanyama mbalimbali, wakiwamo tembo, twiga, nyumbu, swala na viboko waliokuwa wakijidai kwenye bwawa lao la kuogelea.

Meneja Mauzo ya Benki ya TCB, Doroth Lyimo, hakuweza kuzuia furaha yake ya kuona wanawake wengi walivyohamasika na kujitokeza kwa wingi kufanya utalii wa ndani na kutengeza mtandao ambao umerahisisha kuwa na mawasiliano ya karibu.

Amesema, amefurahishwa na hifadhi hiyo kwasababu amebahatika kuona wanyama mbalimbali tena kwa karibu zaidi.

"Vile vile najivunia sana kuwa safari yetu tumeendeshwa na dereva mwanamke wa treni na natamani wangekuwa wengi zaidi nchini," anasema.

Hata hivyo, anashauri safari kama hizo zifanyike mara kwa mara badala ya kutegemea matukio ya msimu kwa kuwa kuna kinamama wanapenda kufurahi kwa kukutana na wenzao katika majumuiko kama hayo.

"Ningependa kuona kila baada ya miezi mitatu zinaandaliwa safari za kwenda kwenye mbuga tofauti zilizopo nchini kwa sababu inatuongezea mtandao wa kufahamiana."

Doroth anasema kiwango cha Sh. 200,000 kilichowekwa kwa ajili ya safari hiyo kimetenda haki kutokana na gharama halisi ya safari kuanzia tiketi, chakula na kutembezwa kwenye hifadhi.

Zena Maulid ni mjasiriamali, ambaye alianza kusikia tangazo la safari hiyo alipokuwa kwenye usafiri wa treni inayofanya usafiri wa umma, maarufu kama 'Treni ya Mwakyembe'.

"Niliposikia tangazo hilo nikahamasika sana, nikasema pamoja na kazi yangu hii ya ujasiriamali nitadunduliza ili na mimi niweze kwenda kufanya utalii wa ndani." Anasema yeye ana nyumba ambayo amepangisha na mmoja wa wapangaji wake anafanyakazi TAZARA, kwa hiyo alimuuliza kuhusu safari na akamwelezea kwa kirefu.

"Hii safari imeniwezesha kujumuika na wanawake wezangu, tazama humu ndani ya treni tupo wanawake wa kila aina, kuna viongozi, wafanyakazi, wafanyabiashara, wajasiriamali, lakini wote tunajiona ni kitu kimoja," anasema.






# Mama adaiwa kuua wanawe wawili kwa kuwanywesha soda yenye sumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia Dainess Mwashambo (30), mkazi wa Kijiji cha Mashesye, Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa tuhuma za kuua watoto wake wawili kwa kuwanywesha sumu.

Inadaiwa kuwa baada ya kutekeleza unyama huo, mama huyo alifanya jaribio la kujiua kwa kunywa sumu hiyo ili kukwepa mkono wa sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga alisema jana kuwa mtuhumiwa huyo aliwaua watoto hao kwa kutumia dawa ya kukaushia majani shambani ijulikanayo kwa jina la Pare Force.

Alitaja watoto waliofariki dunia ni Mario Adamson (4) na mdogo wake wa kike, Beonis Adamson (2. Wote walifariki wakati wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Kamanda Kuzaga alisema chanzo cha tukio hilo ni msongo wa mawazo uliosababishwa na mwanamke huyo kutuhumiwa na serikali ya kijiji hicho kwa wizi, pia aibu iliyotokana na tukio hilo.

Kamanda Kuzaga alisema kuwa Machi 3, mwaka huu, mtuhumiwa alidaiwa kuingia kwenye nyumba ya mwanakijiji mwenzake, Zaria Ndagwa kwa nia ya kuiba vitu ambavyo havikutajwa.

Alisema kuwa mtuhumiwa alikutwa na mwanakijiji mwingine aitwaye Asnat Mapayo ambaye alitoa taarifa kwa mwenye nyumba na ndipo akashtakiwa kwenye serikali ya kijiji.

Alisema kuwa Machi 6, mwaka huu, mama huyo aliitwa na viongozi wa serikali ya kijiji kwa lengo la kumhoji na alikiri kufanya kosa hilo na ndipo wakamtoza faini ya Sh. 25,000 kwa ajili ya gharama za uendeshaji kesi na Sh. 100,000 kama fidia kwa mwenye nyumba alimotaka kuiba.

Alisema mama huyo aliomba viongozi wa serikali ya kijiji hicho apunguziwe adhabu hiyo ili badala ya kulipa Sh. 125,000 alipe Sh. 50,000 pekee, faini ambayo ilikubaliwa na akaambiwa akaitafute.

"Ilipofika Machi 7, mwaka huu, ndipo ikabainika kuwa alikuwa amewanywesha sumu watoto wake kwa kuichanganya kwenye soda na na yeye mwenyewe akawa amekunywa ndipo zikaanza jitihada za kuokoa maisha yao kwa kuwakimbiza hospitalini," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema watoto hao walifariki dunia muda mfupi baada ya kufikishwa katika hospitali hiyo ya rufani na kwamba mama huyo anaendelea na matibabu katika hospitali hiyo akiwa chini ya ulinzi.

Kamanda huyo aliwataka wananchi mkoani Mbeya kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa inasababisha madhara hata kwa watu wasiokuwa na hatia kama ambavyo mwanamke huyo amewaua watoto wake.

Alishauri wananchi wanaopata tatizo la kifamilia, kupata msaada kwa jeshi hilo kupitia dawati la jinsia na watoto au kwa viongozi wa serikali wakiwamo maofisa ustawi wa jamii.

Kamanda Kuzaga alisema mtuhumiwa huyo baada ya kutibiwa na kupona, atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.



Wananchi wakiwa kwenye daraja eneo la Kibutuka mpakani mwa wilaya ya Liwale na Nachingwea mkoani Lindi mwishoni mwa wiki, wakishuhudia uharibifu wa barabara uliosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha mkoani humo.**PICHA:MPIGAPICHA WETU**

## Kesi ya msanii Marioo madai ya milioni 500/- kunguruma

**Na Kulwa Mzee**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Omary Mwanga, maarufu Marioo, anayedaiwa zaidi ya Sh. milioni 500 kwa kuvunja mkataba, anatarajiwa kujitetea Mahakama Kuu Machi 18 na 19, mwaka huu.

Marioo na Meneja wake Sweetbert Mwinula wameshtakiwa katika Mahakama Kuu Masjala ya Wilaya ya Arusha mbele ya Jaji Joackim Tiganga, wakidaiwa jumla ya Sh. 550,000,000 kwa madai ya kuvunja mkataba wa kutumbuiza katika hafla ya Mr & Miss Vyuo Vikuu Kanda ya Kaskazini.

Mdai katika shauri hilo ni Kampuni ya Kismaty inayojihusisha na kuandaa matukio ya burudani mbalimbali nchini.

Mdai anayewakilishwa na Wakili John Lairumbe, anadai kuwa Septemba 23, 2021, aliingia mkataba na wadaiwa kutumbuiza siku ya mashindano hayo kwa gharama ya Sh. milioni 15.

Mdai anadai katika hati yake ya madai kwamba tukio lilitakiwa kufanyika Septemba 24, 2021 Arusha na Septemba 25 mwaka huo kungekuwa na hafla iliyopangwa kufanyika Blue Stone Lounge.

Anadai kuwa kampuni hiyo Septemba 17, mwaka huo, iliwalipa wadaiwa Sh. milioni nane na wakati wakitia saini mkataba, iliwalipa Sh milioni 15.

Inadaiwa kuwa Septemba 25, 2021, hawakuonekana kwa ajili ya kutumbuiza Blue Stone kama walivyokubaliana katika mkataba.

Kutokana na kuvunja mkataba, mdai aliingia hasara ya Sh. 500,000,000 na hasara nyingine ya Sh. 50,000,000 ambayo ilitokana na kukaribisha wadau mbalimbali wakiwamo wenye hoteli kubwa, fedha walizolipwa na alipoteza biashara na kukosa kipato.

# 'Somo la stadi za maisha ndio mkombozi wa mtoto wa kike'

**Na Julieth Mkireri**

SOMO la stadi za maisha kikifundishwa kuanzia shule za msingi litakuwa sehemu ya kukomboa mtoto wa kike kwenye maisha yake ya baadaye.

Meneja Mwandamizi wa Mradi wa Elimu kwa Msichana, Hadija Hassan kutoka Shirika la Room to Read alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema somo hilo pia ni sehemu ya kumpa ujasiri mtoto wa kike katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, hasa kuepuka mimba za utotoni.

Hadija alisema shirika hilo kuwa na mradi unaohusiana na masuala ya wasichana kumekuwa sehemu ya kuwaandaa kukabiliana na vikwazo ambavyo vimekuwa sababu ya wengi wao kushindwa kufikia malengo yao.

Alisema stadi za maisha zinazofundishwa kwenye mradi huo zimekuwa na mabadiliko kwa wasichana kuwa jasiri, ongezeko la ufaulu darasani na kuwa wajasiriamali wanaosaidia wazazi wao kwa kununua baadhi ya mahitaji.

Meneja huyo alibainisha kwamba wasichana zaidi ya 5,000 kutoka katika mikoa ya Pwani, Tanga na Morogoro wamenufaika na Mradi wa Elimu kwa Msichana, uliolenga kutokomeza mila na desturi potovu za ukatili na ukandamizaji wanawake katika jamii.

Kwa mujibu wa Hadija, mradi huo ulianza kutekelezwa katika mikoa hiyo mwaka 2012. Hadi sasa Pwani na Morogoro ndio maeneo ambayo utekelezaji unaendelea kwa shule za msingi na sekondari

Alibainisha kwamba mradi huo umekuwa na mafanikio katika eneo la kupunguza utoro, kuibua ufaulu na kuondoa mimba za utotoni kutokana na stadi tano za maisha wanazofundishwa.

Mmoja wa walimu wa Shule ya Sekondari Bundikani iliyoko Kibaha, mkoani Pwani, Bahati Mgala ambaye yuko kwenye utekelezaji mradi huo, alisema mradi huo umemaliza utoro wa rejareja uliokuwapo awali.

Pia alisema kupitia mradi huo, watoto wa kike ufaulu wao umeongezeka sambamba na kuwa jasiri wa kuhoji maswali kwenye sehemu ambayo hawajaelewa, pia wamekuwa watunzaji fedha wanazopewa kwa ajili ya matumizi shuleni.

Mwalimu Bahati pia alisema halmashauri inatakiwa kuangalia namna ya kujipanga kuwapeleka walimu kujifunza kwenye maeneo unakotekelezwa mradi huo ili kuwa msaada zaidi kwa wasichana walioko shuleni.

Ashura Hamis, mkazi wa Mailimoja, Kibaha ambaye ni mzazi wa Mwajuma Yahaya, mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Bundikani, alishukuru kuwapo mradi huo ambao umemsaidia mtoto wake kuwa na utaratibu wa kuweka akiba na kununua mahitaji ya shule.

Ashura alisema mbali na kuweka akiba, mradi huo umekuwa ukiandaa watoto wa kike na maisha ya baadaye kwa kujifunza ujasiriamali ambao utawawezesha kujiajiri wakiwa likizo na hata baada ya kuhitimu masomo yao.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba, Yanga zijiandae kumpokea yeyote CAF

**DROO** ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika inatarajiwa kufanyika kesho Jumanne jijini Cairo, Misri, ambapo wawakilishi wa Tanzania, Simba na Yanga watafahamu timu zipi watakazokwenda kukutana nazo kuanzia Machi 29-31, mwaka huu.

Kuna mijadala inatembea mitaani na mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari, kuonyesha ni timu ipi yenye afadhali kwa wawakilishi hao wa nchi, kukutana nayo kuliko nyingine.

Lakini hapa tunataka kuweka wazi kwa viongozi, wanachama na mashabiki wa timu hizo kutojidanganya kuwa kuna timu dhaifu au yenye uafadhali kwenye hatua hiyo.

Hakuna timu dhaifu ambayo inaweza kuingia kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika kwani timu zote dhaifu zilitolewa hatua za mwanzo na huku kulikobaki ni kwa wakubwa kuwa tayari kupamba na timu yoyote ile.

Tukianza na Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri, hii ndiyo timu hatari zaidi kukutana nayo, hasa kwenye hatua kama hizi za mtoano na hii kuna nafasi pia kukutana na Simba.

Ndiyo timu iliyotwaa ubingwa mara nyingi kombe hilo barani Afrika, na hata ikitolewa basi mara nyingi inakuwa ni fainali.

Asec Mimosas ya Ivory Coast siyo timu ya kuichukulia poa kwani mpaka inafuzu ilikuwa haijafungwa mechi yoyote, ikiwa ni moja kati ya timu chache za mwanzo zilizofuzu mapema tu, na hata ilipopoteza mechi ya mwisho ugenini dhidi ya Wydad Casablanca kwa bao 1-0, kulikuwa na maswali mengi kutoka kwa mashabiki juu ya kiwango chao siku hiyo na namna goli hilo lilivyofungwa, hii pia ni moja kati ya timu inayoweza kukutana na Yanga.

Mamelodi Sundowns hii ndiyo timu ambayo inaogopwa na Watanzania wengi kutokana na rekodi yao nzuri ya hivi karibuni, huku mashabiki wa timu hizo wakiihofia zaidi kukutana nayo na inaweza kukutana na Simba ama Yanga.

Kuna timu isiyoimbwa, nayo ni Petro de Luanda ya Angola, iliyomaliza mechi zake sita za Kundi C, si tu kwamba haikupoteza hata mechi moja, lakini haikuruhusu bao.

Imecheza mechi sita, ikishinda michezo mitatu na sare tatu pia, ambapo awali ilionekana mashabiki wa timu hizi wangependa kukutana nayo, lakini rekodi zimeanza kuwatisha na yenyewe inaweza kukutana na Simba ama Yanga.

Hivyo wakati droo inakwenda kuchezeshwa, Simba na Yanga zitumie michezo hii ya Ligi Kuu kuangalia mapungufu yao na kuyarekebisha kabla ya mechi hizo, hasa ya kushindwa kutumia nafasi.

Kwenye michezo ya Ligi Kuu, timu hizo zimeonekana kutengeneza nafasi nyingi, lakini zikishindwa kutumia, hivyo ni fursa kwao kurekebisha kasoro hizo na si kuanza kuota ndoto za kutaka kupangwa na timu fulani.

Zikumbuke kuwa kwenye hatua kubwa kama hizo, zisitarajie kama zinaweza kupatikana nafasi nyingi kama zinazotengenezwa kwenye Ligi Kuu. Tunatambua kuna wachezaji wenye viwango vya hali ya juu, hivyo nafasi huwa chache, kinachotakiwa ni kuzitumia na kuhesabu mabao.

Aidha, ikumbukwe pia kwa mujibu wa kanuni, timu zote za Tanzania zitaanzisha nyumbani, hivyo kinachitakiwa ni kuimaliza mechi hapa hapa kwa kushinda mabao mengi na hiyo itawezekana tu pale zitakapojipanga kwenye maandalizi ya kiufundi.

Tunaamini kama ikija timu ikifungwa mabao 4-0, kama ilivyofungwa CR Belouizdad ya Algeria, sidhani kama kutakuwa na kupindua meza ugenini kwa timu kama Yanga ambayo hata ugenini inacheza kama nyumbani tu.

Kadhalika kwa Simba ikishinda mabao 6-0 kama ilivyoifanya Jwaneng Galaxy ya Botswana, au 7-0 kama ilivyochapika Hoyoya ya Guinea, msimu uliopita, hatudhani kama ikienda ugenini inaweza kutetereka, kwani hivi sasa ni moja kati ya klabu kubwa barani Afrika yenye uwezo wa kukwepa hujuma zote inapokwenda kucheza ugenini.

Kwa ujumla Nipashe tunawataki kila kheri wawakilishi hao wa nchi katika maandalizi yao kwa kuwa hicho ndicho kitu cha muhimu kuliko vingine vyote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Tatizo la taa viwanja vya soka mikoani lifanyiwe kazi

Na Adam Fungamwango

**BAADA** ya idadi kubwa ya mashabiki kuangalia mechi mbili za Simba na Yanga zilizochezwa usiku katika viwanja tofauti vya mikoani, wameonekana kulalamikia taa kuwa zina mapungufu.

Yanga ilicheza dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi Ijumaa iliyopita, kuanzia saa 12:00 jioni, na juzi Simba ilikuwa Uwanja wa Mkwakwani, Tanga ikicheza dhidi ya Coastal Union.

Mechi hiyo nayo ilianza saa 12:00, lakini zote zilionekana taa zilizofungwa kwenye viwanja hivyo ni za aina moja.

Na siyo viwanja hivyo tu, binafsi hata ukiangalia taa za viwanja vya Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera, Jamhuri Dodoma, vyote hivyo vinaonekana kuwa na matatizo.

Ni tofauti kabisa ukiangalia mechi Uwanja wa Benjamin Mkapa na ule wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Ubora wa taa za viwanja hivyo viwili, au mtu aliyezoea kuangalia mechi kwenye viwanja hivyo, wala hatotumia ujuzi wowote kung'amua kuwa kuna tofauti ya ubora wa taa.

Nikisema hivyo sina maana kuwa waliokuwa uwanjani hawaangalii vizuri mpira, au wachezaji ndani wanashindwa kucheza ama kuna maeneo hawaoni, la hasha.

Tatizo la taa linaloonekana ni kwa wale walioangalia mechi kupitia televisheni. Hawa ndiyo wanaathirika mno na mechi zinazochezwa kwenye viwanja vya mikoani.

Kwa kiasi kikubwa watazamaji wanachoona zaidi ni wachezaji kuliko mpira. Huonekana tu pale wachezaji wanapovutwa na kuonekana wakubwa.

Kasheshe ni pale wachezaji wanapokuwa kwenye saizi ya kwaida ya kuonyesha mpira kama ilivyozoeleka, mpira hauonekani, unachoweza kuona wachezaji wanakimbiakimbia.

Watazamaji sasa wanakuwa wanamtegemea zaidi mtangazaji ili kujua mpira uko wapi, kama umeshapigwa krosi, shuti, umeokolewa au kipa kadaka.

Narudia tena, hili huwezi kuliona kwenye viwanja wa Benjamin Mkapa au Azam Complex, hata mpira ukichezwa usiku wa manane.

> **Nikisema hivyo sina maana kuwa waliokuwa uwanjani hawaangalii vizuri mpira, au wachezaji ndani wanashindwa kucheza ama kuna maeneo hawaoni, la hasha.**

Binafsi, nimeliona hilo, lakini hata mashabiki wengi wameonekana kulalamikia hilo, hivyo naliwasilisha kwa wahusika ambao ni Bodi ya Ligi nchini, TPLB.

Inaonekana kabisa kuwa aina ya taa zilizofungwa, pamoja na dhamira njema, lakini wataalam hawajaangalia kama zinaweza kuoana na miale ya taa zingine zilizopo kwenye televisheni za majumbani na mionzi yake inapokutana na macho ya binadamu.

Kuangalia soka ni burudani, ambapo kwa sasa limebeba mashabiki wengi, wake kwa waume na watoto, hivyo kasoro kama hizi ni lazima ziangaliwe na kurekebishwa mbele ya safari.

Nimeona baadhi ya wachambuzi walikuwa wakiorodhesha kasoro mbalimbali kwa wenye mamlaka ya kuonyesha mpira kwenye televisheni, ikiwamo picha za marudio, engo za kukaa na vitu vingine vya kiufundi kwa hiyo wakati hayo yakifanyiwa kazi, na hili suala la taa nalo liangaliwe kwani linakera.

Kwa Watanzania wengi ambao wamezoea kuangalia mechi mbalimbali za ligi barani Ulaya ambapo mpira unaonekana mpaka nembo yake, achilia mbali ubora wa taa za uwanjani na uonyeshaji wenyewe, leo wanakutana na mechi inayochezwa Mkwakwani au Majaliwa, halafu anaona watu wanakimbia, mpira wenyewe hauoni, sidhani kama atafurahi.

Kama tunasema Ligi ya Tanzania ni namba sita kwa sasa kwa ubora Afrika, basi kuna vitu vingi vya kuvitazamani ikiwamo ubora wa taa zetu za uwanjani.

Nafikiri pia walioweka taa hizo ndiyo hawa hawa ambao wamedhamini ligi kwa kuionyesha, hivyo kuna vitu vya kitaalam vya kufanya ili mechi zinazochezwa usiku zionekana katika ubora unaotakiwa na isiwe kama mpira wa vikatuni.

HABARI KITAIFA

## Zone-KiSEZ yachangia uchumi viwanda Kigoma

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Kigoma (Kigoma Special Economic Zone-KiSEZ) imechangia kuvutia wawekezaji, kuzalisha ajira na maendeleo ya viwanda katika Mkoa wa Kigoma.

KiSEZ ni kampuni ya serikali iliyopewa leseni na Mamlaka ya Eneo Huru la Uwekezaji kwa Mauzo Nje (EPZA) ambako kwa sasa kuna viwanda sita, vitatu vikiwa vinafanya kazi na vingine katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa KiSEZ, Sangu Deogratius, alisema mwishoni mwa wiki kuwa serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 600,000 ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi.

"Kutokana na ongezeko la wawekezaji katika eneo la KiSEZ, mchango wake katika maendeleo ya viwanda na uchumi wa Mkoa wa Kigoma umekuwa ukiongezeka kwa kiasi kikubwa," alisema.

Kampuni ya KiSEZ ilianzishwa mwaka 2013 kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye viwanda mkoani Kigoma na pia kukuza biashara na mikoa ya jirani na nchi za Maziwa Makuu.

Ongezeko la uwekezaji wa viwanda katika eneo hili utachangia zaidi kuzalisha kazi kwa wakazi wa mkoa huu, kupata mafunzo na ujuzi mbalimbali, na kulipa kodi mbalimbali za serikali.

Mmoja wa uwekezaji mkubwa ambao umepata leseni kutoka kwenye mamlaka ya EPZA ni kiwanda cha kuchakata asali cha Thirdman Company Limited. Meneja wa Operesheni, Ziman Mbena alisema, kiwanda hiki kilichoanzishwa mwaka 2018 na kilizalisha tani 40 kwa mwaka. Lakini hadi kufikia mwisho wa mwaka jana uzalishaji ulifikia tani 1,000 na kwa mwaka huu malengo ni kuzalisha tani 1,800.

Kiwanda hicho cha kuchakata asali kimeajiri watu 60 kwa ajira za moja kwa moja na kufanya kazi na wafugaji wa nyuki zaidi ya 1400 katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Singida.

Alisema katika kuhakikisha ubora unazingatiwa, kiwanda kimewaingiza wafugaji nyuki kwenye kanzi data kwa ajili ya kufuatilia uzalishaji wa asali unaozingatia viwango vinavyotakiwa katika soko.

Pia, wanatoa mafunzo kwa wafugaji wa nyuki ili kuweka na kuzingatia mazingira ya ubora katika ufugaji wao.

Alisema masoko makubwa ya bidhaa za asali ni pamoja na Afrika Kusini, Norway, Sweden, Amerika na Australia.

Kiwanda kingine ni NexGen Solawazi Limited ambacho huzalisha umeme wa megawati tano na kuwauzia Tanesco kwa ajili ya kusambaza sehemu mbalimbali za mkoa wa Kigoma.

Mkoa wa Kigoma haujaunganishwa na gridi ya Taifa, umeme huo umekuwa chachu kubwa katika maendeleo ya viwanda na shughuli nyingine za kiuchumi za mkoa huo.

Msimamizi Msaidizi wa kiwanda, Augustine Mabuga, alisema umeme huo umepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uzalishaji kwa kutumia mafuta kwa takribani Shilingi bilioni sita kwa mwaka.



Mwonekano wa sehemu ya ufukwe wa Rainbow, Mbezi Beach, Dar es Salaam. **PICHA: JENIFER GILLA**

# Wafanyabiashara walalamika plastiki kuchafua fukwe Dar

**Na Jenifer Gilla**

LICHA ya juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na wadau wa mazingira kuweka fukwe katika hali ya usafi jijini Dar es Salaam, tatizo la utupaji wa taka hizo limeendelea kuathiri biashara kwa wawekezaji wadogo wa maeneo hayo.

Ripoti ya Muungano wa Kimataifa wa Kuhifadhi Mali Asili (IUCN) kuhusu plastiki na jamii za ufukweni nchini ya mwaka 2021 inaonyesha kuwa asilimia 40 ya taka hizo zinakusanywa, lakini asilimia 96 hazisimamiwi na kusababisha kuingia kwenye mabwawa, bahari na maziwa.

Nipashe ilitembelea katika ufukwe wa Raibow, Mbezi Beach na Msasani jijiji Dar es Salaam, maarufu kama Beachmavi na kukuta taka za plastiki zimezagaa huku wafanyabiashara wakilalamikia hali hiyo kuathiri shughuli zao.

Mfanyabiashara wa vinywaji katika ufukwe wa Rainbow, Ramadhani Juma, alisema kwa sasa biashara yake imedhorota ikilinganishwa na miaka sita iliyopita wakati anaanza kwa sababu watu hawatembelei fukwe hiyo kutokana na uchafu.

Alitaja aina za taka zilizoshamiri kuwa ni taulo za kike, diapers (nepi za watoto), chupa na mifuko ya plastiki, taka za hospitali kama mabomba ya sindano na chupa za drip jambo linalohatarisha mazingira na afya za wanadamu.

"Zamani angalau watu walikuwa wanapita eneo hili kupunga upepo ufukweni wananunua vinywaji sasa hivi hakuna watu kwa kuwa hii fukwe imejaa taka za plastiki pia zimezagaa," alisema.

Juma mwenye familia ya watoto watatu alisema wakati anaanza biashara hiyo alikuwa anauza kreti mbili za soda kwa siku, lakini sasa hivi anauza nusu kreti.

Mfanyabiashara mdogo wa chakula katika ufukwe wa Beachmavi, Zuhura Magimbe, alisema wateja wamepungua na waliobakia ni wavuvi wanaofanya shughuli zao eneo hilo.

Alisema wakati anaanza biashara katika eneo hilo mwaka 2015 alikuwa anauza hadi kilo tano na kilo tatu za ugali kwa siku kwa kuwa watu mbalimbali walikuwa wakitembelea eneo hilo, lakini sasa anauza wali kilo mbili na ugali kilo mbili.

"Watu sasa hivi hawaji tena kama zamani, taka zimekuwa nyingi hasa kipindi cha mvua, lakini pia kuna mifumo imewekwa inamwaga maji machafu katika eneo hili kwa hiyo maji ya bahari ni meusi hayana mvuto na harufu ni kali," alilalamika.

Wakati mamalishe, Jacline Joseph alisema moja ya changamoto anayokutana nayo katika biashara yake ni wateja kuchagua mboga, wengi wakikataa kula samaki wakiamini kuwa si salama kutokana na madhari ya fukwe hiyo.

"Wateja wengi hasa wanaopita njia, wakija hapa wanakwambia kama hauna mboga nyingine basi, ila samaki hapana, ukiwauliza sababu wanasema hayo maji machafu ya habarini huyaoni, hao samaki hawatokuwa salama kwa afya zetu," alisema.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mzingira, Mbezi Beach A, Karoline Ngoda, alisema uchafu katika eneo hilo unachangiwa na Mto Mbezi pamoja na mito mingine iliyopo katika jiji hilo, inayomwaga maji baharini.

Alisema huandaa utaratibu wa kusafisha fukwe hizo mara kwa mara kwa kushirikiana na wadau, lakini baada ya muda mfupi taka hizo zinarudi tena hasa kipindi cha mvua.

Aliiomba serikali kuweka chujio katika mito inayotiririsha maji ili kuzuia taka kuingia katika bahari.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mikakati ya Maendeleo Endelevu (TSDI), Fredy Kwezi, alisema pamoja na juhudi kubwa wanazofanya wadau wa mazingira kusafisha fukwe hizo hali haibadiliki jambo linalokatisha tamaa.

Alisema kama ufukwe huo ukiwa katika hali ya usafi utakuwa chanzo kizuri cha kuiingizia serikali mapato na kuwanufaisha wafanyabiashara wadogo wa eneo hilo na kuiomba serikali itilie mkazo kuboresha hali ya usafi katika eneo hilo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), Sarah Pima, alishauri jamii kufuata Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kifungu namba 106 inayotaka mtu yeyote kutochafua mazingira au kuruhusu mtu mwingine kufanya hivyo.

Aidha, amewakumbusha viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya mtaa kutekeleza maagizo ya sheria ya mazingira mwaka 2004 kifungu namba 1(a) inayowaeleza kuhakikisha taka zote zinaainishwa na kuchambuliwa kuanzia ngazi ya familia zinakozalishwa.

Alisema kwa kufanya hivyo itasaidia taka hizo hasa za plastiki kutotupwa ovyo na kuzagaa mitaani hali zinazosababisha kuingia kwenye mitaro ya maji na kuishia baharini.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Walimu kufanya mtihani kabla ya kuajiriwa

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imesema katika kutekeleza mitaala mipya ya elimu, walimu wapya watafanya mtihani kabla ya kuajiriwa na watakaofanya vizuri ndio watakaopata nafasi serikalini.

Pia imesema walimu walioko kazini kwa sasa wataendelea kupewa mafunzo ya mara kwa mara ili kuondokana na changamoto katika utekelezaji Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 214 Toleo la 2023 na mitaala mipya.

Utaratibu wa mitihani kwa watumishi kabla ya kuajiriwa, kwa mujibu wa serikali, ni jambo la kawaida katika kada mbalimbali kama sheria na afya.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokutana na wahariri na waandishi wa habari kuelezea sera na mitaala mipya ya elimu na mafanikio katika sekta ya elimu kwa miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.

Alisema serikali imelazimika kuweka utaratibu huo kutokana na wingi wa uhitaji wa ajira za ualimu na kwamba mpango huo utasaidia kuondoa lawama dhidi ya wabunge majimboni na viongozi wengine.

"Sasa hivi walimu ni wengi, ukitangaza ajira hapa ni 'vita'. Watu wakisikia ajira zimetangazwa kila mtu anaomba msaada binafsi ana mtu wake. Sasa tukisema kigezo gani kitumike kama wameomba 10,000, tunahitaji 2,000 tunachaguaje hawa?

"Kutokoana na changamoto hiyo, tukaona tuweke utaratibu wa kuwafanyia uthamini kuwapa mitihani na watakaofaulu wataajiriwa. Ukiona umekosa, unaweza kukata rufani ili mtihani wako usahihishwe tena. Hii itaondoa kelele za mbunge wa jimbo fulani kuulizwa ajira za walimu," alisisitiza.

Prof. Mkenda aliongeza kuwa: "Kinyume cha utaratibu huo, tunakwenda kuua elimu. Wanaosoma sheria sisi wenyewe tunawapa mtihani wanafanya, wakifaulu wanaingia kwenye ajira. Udaktari pia sisi ndio tunawapa mtihani wnafanya, wakifaulu wanapata ajira.

"Wako walimu waliosoma nje nafasi zikiwapo si wote tuwachuje kwa uwezo wao au tuwape tu ajira? Hilo ndio linaleta zogo ndio maana nimeona niliseme hili kuondoa mkanganyiko."

Kuhusu Sera ya Elimu na mitaala mipya, waziri huyo alisema huo ni mpango wa mageuzi ya elimu unaotokana na R4 za Rais Samia na kwamba yeye ndiye alitaka wananchi washirikishwe katika kutoa maoni yao ili yazingatiwe katika maboresho hayo.

Alisema kwa mwaka huu imeanza mitaala mipya kwa elimu ya awali, darasa la kwanza na la tatu, elimu ya sekondari kidato cha kwanza kwa shule zenye mkondo wa amali, vyuo vya elimu na kidato cha tano.

"Tumefanya hivyo baada ya majadiliano marefu, unaweza ukajiuliza darasa la tatu mbona hawapo, tuliona elimu ya awali na darasa la kwanza si shida wanaweza wakaanza na mitaala mipya.

"Lakini darasa la tatu watakuwa na muda wa kukacha yale ambayo walitakiwa kusoma darasa la pili na wataendelea na mitaala hiyo mpaka pale watakapomaliza elimu yao.

"Na wale wa zamani wa darasa la pili wakiingia la tatu pia wataendelea na elimu ya mitaala mipya, na hao wa darasa la tatu wakiingia darasa la nne wataendelea na elimu yao mpaka darasa la sita, mwaka 2027 watakuwa darasa la sita kwa kuwa mitaala mipya elimu ya msingi ni miaka sita na si saba," alifafanua.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (wa pili kushoto) akimpatia tuzo Mjiolojia kutoka GGML, Janeth Luponelo kutokana na mchango wa kampuni hiyo katika masuala ya jinsia. Kushoto ni Waziri wa Madini, Anthony Mavunde. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usawa kijinsia waundiwa mkakati maalum mgodini

**Na Mwandishi Wetu**

USHIRIKI wa wanawake katika sekta ya madini ni mdogo kutokana na sababu mbalimbali.

Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imeliona hilo na kuweka mkakati maalum wa kisera kuongeza ushiriki wa kundi hilo mgodini.

Uongozi wa kampuni hiyo umesema moja mambo yaliyowezesha mgodi wake kuongoza nchini kwa kuongeza kuwa na idadi kubwa ya wanawake walioajiriwa kwenye sekta ya madini, ni kubuni na kutekeleza kwa vitendo sera na miongozo inayohamasisha usawa wa kijinsia maeneo ya kazi.

Mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Makamu Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu na masuala ya ushirika Afrika, Simon Shayo, alibainisha hayo katika sherehe za awali za kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Shayo alisema hivi sasa asilimia 13 ya nguvukazi ya kampuni hiyo ni wanawake ilhali kwa upande wa kimataifa ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini, takwimu zinaonesha ni kati ya asilimia 14 na 16.

"Hivyo, hatufanyi vibaya. Tuliendesha mgodi bila kuwapo wanawake katika nafasi za juu za uongozi lakini sasa wapo na wengine wamevuka mipaka na kwenda kuwa wasimamizi wa sekta hiyo katika kampuni mbalimbali nje ya nchi," alisema.

Shayo alisema sera na miongozo ya GGML iliyowekwa si kwamba imeongeza idadi ya wanawake kushiriki kwenye shughuli za mgodi huo, bali pia imebadilisha hulka za wanaume waliopo kwenye kampuni hiyo na kuona umuhimu wa wanawake kuwapo kwenye sekta ya madini.

Shayo alitaja baadhi ya miongozo hiyo kuwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kuajiri ambao unatoa kipaumbele kwa wanawake.

"Katika ajira asilimia 50 ni wanawake na asilimia inayobaki 50 ni wanaume na kama watalingana ufaulu katika usaili anayepewa kipaumbele ni mwanamke," alisema.

Aliongeza kuwa kampuni hiyo pia hutoa ufadhili kwa wafanyakazi wake wanawake kwenda kupata mafunzo ya juu ya uongozi yanayotolewa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) ambapo tangu mafunzo hayo yaliyopewa jina la Female Future Program (FFT), yaanze mwaka 2016, wanawake 23 kutoka GGML wamefadhiliwa na kuhitimu mafunzo hayo.

"Pia ndani ya mgodi tuna mwongozo unaoitwa 'don't cross the line', kwamba usivuke mpaka au mstari kwenda kumghasi, kumtendea ukatili wowote mwanamke na kama kukitokea jambo lolote kuna namba za simu za kutoa taarifa kwa njia ya siri na hatua kuchukuliwa," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye hafla hiyo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa alisema kampuni za madini zinatakiwa kuzingatia kanuni ya 'Local Content' (kununua na kutumia bidhaa/huduma za ndani katika uendeshaji wa kampuni) iliyopo kwenye mabadiliko ya sheria ya madini kwa kuzingatia ushirikishwaji wanawake kwenye masuala ya ununuzi.

Alisema kipengele hicho cha ushirikishaji wazawa katika mnyororo wa thamani, pia ni fursa nzuri kwa kampuni za madini kushirikisha wanawake katika ununuzi mbalimbali ambao unatengewa bajeti kubwa kuliko hata kodi zinazolipwa kwa serikali.

"Wanawake wanaojishughulisha kwenye shughuli za sekta ya madini wamekuwa na mchango mkubwa katika kujenga uchumi wao na Pato la Taifa," alisema Waziri Slaa.

# Elimu ya sheria za ardhi, ndoa na mirathi yatolewa kwa wanawake

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANAWAKE wilayani Kilosa, mkoani Morogoro wamepatiwa elimu kuhusu sheria zinazohusu mirathi, ardhi na ndoa kupitia mpango wa kusaidia jamii katika masuala mbalimbali ya kisheria chini ya Mpango wa Kituo cha Msaada wa Kisheria cha Chuo Kikuu Mzumbe (MU).

Mhadhiri wa Sheria wa chuo hicho, Dk. Thobias Nyamsenga, alisema wanawake hao walipatiwa elimu hiyo baada ya wataalam wa Mzumbe kuweka kambi ya siku tatu katika wilaya hiyo.

Dk. Nyamsenga alisema Mzumbe kupitia watalaam wake kutoka Kitivo cha Sheria waliamua kutoa bila malipo huduma ya msaada wa kisheria kwa wanawake hao pamoja na waliopatwa na majanga mbalimbali ikiwamo ya mafuriko.

Alisema kambi hiyo ya kutoa msaada huo wa kisheria imelenga kusikiliza wananchi na kuwapatia msaada wa kisheria kwa wale wasiojiweza husussani ushauri katika maeneo matatu ambayo ni eneo la mirathi, ndoa na ardhi.

Alisema jamii ina uelewa mdogo kuhusu masuala ya mirathi. Hilo limekuwa linasababisha migogoro ikiwamo ya ardhi.

Alisema waathirika wakubwa wa migogoro hiyo ni wanawake kwa kuwa baadhi ya wanafamilia humiliki mali kienyeji na kusababisha kuwapo migogoro hiyo.

"Tumeweka kambi ya siku tatu na tumepokea wateja wa kutosha na kwa idadi kubwa katika masuala hayo matatu ambayo ni mtambuka katika Wilaya ya Kilosa," alisema Dk. Mnyasenga.

Mhadhiri na Mratibu wa Kituo cha Msaada wa Kisheria Chuo Kikuu Mzumbe, Wakili Bernadetha Iteba, alisema kituo hicho kinajihusisha na kutoa msaada wa kisheria bila malipo kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kumudu gharama za kisheria na kuwalipa mawakili na watu wa aina hiyo wanapokewa katika kituo hicho.

Alisema kituo pia kinatoa msaada wa uwakilishi mahakamani kwa kesi ambazo ni nyeti baada ya kuona mwananchi huyo asipopewa wakili wa kwenda kumsaidia na kumsimamia mahakamani, anaweza kupoteza haki, hivyo kituo kinampa wakili bila malipo kusaidia na kumsimamia.

Kaimu Makamo Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Allen Mushi, alisema pamoja na kutoa elimu kuhusu sheria, wametumia Siku ya Wanawake Duniani kutoa misaada mbalimbali kwa waathirika wa mafuriko wilayani humo.



# Mchakato KCBL kuwa Benki ya Taifa ya Ushirika waiva

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NDOTO ya vyama vya ushirika nchini kumiliki benki yao ya taifa imetimia rasmi, baada ya Menejimenti ya Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL), kutangaza kwamba Rais Samia Suluhu Hassan, ameridhia benki hiyo kuwa Benki ya Taifa ya Ushirika (NCBT)

Kabla ya kufikiwa kwa vigezo vya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) vya kuundwa kwa NCBT ili kuingia kwenye ushindani wa tasnia ya biashara za kibenki, KCBL ilitakiwa kuwa na mtaji wa Sh. bilioni 15.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati KCBL ilipoungana na wafanyakazi wa benki hiyo kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Kaimu Meneja Mkuu wa KCBL, Frank Wilson, alisema Rais Samia, ataizindua benki hiyo kati ya Mei au Juni mwaka huu katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

"Tunatazamia kuizindua benki hii Mei au Juni mwaka huu. Benki hii imekuwa ikiheshimu sana mchango wa wanawake kama ambavyo leo tunaadhimisha hii Siku ya Wanawake Duniani.

"Wakati tunarejea sokoni mwaka 2020 baada ya benki yetu kuyumba, tulikuwa na mtaji wa shilingi bilioni 2.2 na hadi kufikia mwaka 2023, mtaji wetu ulikuwa umefikia Sh. bilioni 16.

"Kwa upande wa mali, wakati tunarejea sokoni tulikuwa na shilingi bilioni nane, lakini mpaka kufikia mwaka jana tulikuwa na Sh. bilioni 25.

Kwenye amana za wateja kwa maana ya akiba za wateja, wakati tunaanza operesheni tulikuwa na Sh. bilioni 5.2 lakini mpaka kufikia Desemba tulikuwa tuna Sh. bilioni 9.1" alisema.

Kwa mujibu wa Frank, Katika mikopo, wakati wanarejea sokoni walikuwa na mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 264, lakini mpaka kufikia mwaka 2023, walikuwa wametoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 8.8

Alisema kwa upande wa faida, wakati wanaanza operesheni, walitegemea kupata hasara ya Sh.bilioni 1.5, lakini baada ya utendaji mzuri walipata hasara ya Sh. milioni 600.

Katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Utawala, Pendo Mabula na Meneja wa Tawi wa KCBL, Neema Soka, waliwasilisha mwenendo wa benki hiyo pamoja na bidhaa nyinginezo za benki.



Mbunge wa viti maalum mkoa wa Manyara, Regina Ndege (katikati) amekabidhi viti mwendo kwa watoto walemavu watatu wa Wilaya ya Mbulu, wapili kulia ni mbunge wa Mbulu vijijini Flatei Massay, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake wafanya usafi Bwawa la Maji Kwamaizi

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

KATIKA maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, wanawake wa Kata ya Kideleko katika Halmashauri ya Mji wa Handeni mkoani Tanga wamepanda miti na kufanya usafi katika Bwawa la Maji la Kwamaizi.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Handeni (HTM), Yohana Mgaza, alisema kuzinduliwa kwa bwawa hilo limewasaidia wanawake kutokufuata maji umbali mrefu.

"Toka kuzinduliwa kwake mwaka jana, Bwawa la Kwamaizi limekuja ni mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Kata ya Kideleko hasa kinamama ambao wao ndiyo wana jukumu la kutafuta maji kila siku,"alisema Mgaza.

Bwawa la Kwamaizi katika Halmashauri ya Handeni lilikamilishwa chini ya ufadhili wa kampuni ya bia ya serengeti na kusimamiwa na shirika lisilo la kiserikali la WaterAid, tangu lilipokamilika mwaka jana linahudumia takribani wananchi 1900.

Akizungumzia nafasi ya kinamama katika usimamizi wa miradi ya maji na usafi wa mazingira, mwakilishi wa Mkurugenzi wa WaterAid Tanzania, Neema Kimaro alisema licha ya mradi huu kulenga huduma ya maji safi kwa wananchi, kuliundwa kikundi maalum cha kinamama 24 waliosajiliwa kwa kazi maalum ya kuwezesha jitihada za kusimamia masuala yote ya uhifadhi wa mazingira na ulinzi wa miundombinu ya maji ikiwemo usafi katika bwawa.

Mwenyekiti wa kikundi cha kinamama wanaosimamia mradi huo, Fransisca Mhando, alisema lengo la kikundi ni kusimamia mauzo ya maji katika bwawa hilo, matunzo na usafi wa mazingira katika eneo linalozunguka bwawa.

# Shule 30 Vunjo zapewa msaada taulo za kike

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

WANAFUNZI wa kike 1,440 kutoka shule 30 za Jimbo la Vunjo lililoko Moshi, mkoani Kilimanjaro, wataondokana na adha ya kukosa masomo yao kila mwezi kutokana na kukosa taulo za kike za kujisitiri wakati wa hedhi baada ya kupewa msaada.

Takwimu za Wizara ya Elimu, zinaonyesha kuwa wanafunzi wa kike walio katika mazingira hayo, hukosa masomo kati ya siku tano hadi saba kila mwezi, sawa na siku 60 hadi 70 kwa mwaka.

Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, akizungumza mwishoni mwa wiki na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mieresini iliyoko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo, alisema ameamua kubeba jukumu hilo ili kuhakikisha wanafunzi hao wanazifikia ndoto zao za kupata elimu.

Dk. Kimei, aliyewakilishwa na Katibu wake, Gulatone Masiga aliitumia siku hiyo kama sehemu kuunga mkono maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

"Niwaombe wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu katika kuwawezesha watoto wa kike kuyafikia malengo yao, kwa kutoa mahitaji muhimu zikiwemo taulo za kike.

"Iko haja kwa jamii kujitokeza na kuvunja ukimya kuhusu hedhi salama, kuanzia ngazi ya familia ili kuwasaidia watoto wa kike hasa wenye ulemavu kufahamu mapema namna ya kujisitiri." alisema

Dk. Kimei alisema licha ya serikali kulipa kipaumbele suala la hedhi salama kwa mtoto wa kike, bado jitihada za wadau zinahitajika ili kufikia azma hiyo kutokana na baadhi ya wazazi/walezi kushindwa kumudu mahitaji hayo.

Mmmoja wa walimu wa Shule ya Sekondari Mieresini, Julieth Munisi, alisema kutokana na uchache wa taulo hizo imekuwa ni tatizo kubwa kwa watoto wa kike, wanapokuwa shuleni kwa kuwa hushindwa kijisitiri.

# RC aiangukia WFP kurejesha mpango wa lishe shuleni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ameliangukia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), kurejesha mpango wa lishe kwenye shule za pembezoni zinazotumiwa na jamii za wafugaji wa kimasai, ili kuwanusuru wanafunzi wa maeneo hayo dhidi ya utapiamlo.

Mongela, aliwasilisha ombi hilo la serikali mwishoni mwa wiki wakati akizindua ofisi za WFP. Mongela, aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Kanali Wilson Sakulo,

Alisema miaka ya nyuma, WFP walikuwa wakitoa chakula kwenye shule za pembezoni, hasa zile zinazotumiwa na jamii za wafugaji na ziliongeza ufaulu, uelewa na kupunguza utoro shuleni.

Alisema hali hiyo inatokana na mabadiliko ya tabianchi, ambayo yamesabisha ukame na mafuriko ya mara kwa mara, yanayoathiri shughuli za kilimo na mifugo katika maeneo hayo.

"Mbali na kusababisha athari katika kilimo na mifugo, pia wanyamapori huathiriwa na ukame, ambao ndio chanzo cha utalii unaoleta kipato kwa wanaanchi wa mkoa huu na taifa kwa ujumla.

"Nawaomba WFP, fikirieni jinsi ya kurudisha mpango endelevu wa lishe shuleni maeneo haya kwa kushirikiana na serikali, wadau na wazazi. Serikali inatambua juhudi za WFP za kushirikiana na serikali na walengwa katika kutatua changamoto za mabadiliko ya tabianchi yanayoleta athari ya utapiamlo.

Zaidi aliongeza: "Lakini tunatambua jitihada zenu za kusaidia wakulima wadogo kupata pembejeo bora na kwa wakati, kupata masoko ya mazao na kupunguza upotevu wa mazao yao baadabya kuvuna."

Mkurugenzi Mkuu wa WFP, Sarah Gordon, alisema uwepo wa ofisi yao utasaidia kutekeleza mpango wao wa kusaidia vijana katika kilimo cha biashara na ufugaji na kukuza hali zao za kiuchumi.

Vilevile, alisema wadau wanapaswa kuwawezesha na kutoa sauti kwa wanawake na vijana iwapo wanataka kuleta mabadiliko ya kudumu katika maisha yao, Tanzania ifikie maendeleo jumuishi na endelevu.





# Madadapoa wageuka tishio mgodini, wachimbaji wajawa hofu

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

ONGEZEKO la wadada wanaouza miili yao, maarufu dadapoa katika mgodi wa wachimbaji wadogo wa Chapakazi and Partners Gold Mine uliopo Kijiji cha Wisolele, Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, limekuwa tishio na kuwatia hofu wachimbaji.

Kufuatia hali hiyo baadhi ya wachimbaji mgodini hapo wameiomba serikali kutuma timu ya watalaamu wa afya ambao watawapatia elimu ya kujikinga na UKIMWI ili kuwanusuru vijana wa eneo hilo.

Akizungumza na Nipashe mgodini hapo, Katibu wa Mgodi huo, Stephen Lutego alisema kwa sasa wameingiwa na hofu ya kusambaa kwa virusi baada ya kuongezeka kwa madadapoa wanaojiuza majira ya jioni baada ya kazi.

Alisema idadi kubwa ya wachimbaji hao hawana elimu hiyo, hivyo kufanya ngono zembe mara kwa mara na madadapoa hao hali inayohatarisha afya zao.

"Wadada hawa wanatoka mikoa mbalimbali hapa nchini na wanafanya biashara ya kuuza miili yao kwa wachimbaji wetu, tunaomba mamlaka husika kulifanyia kazi hili suala,"alisema Lutego.

Mkaguzi wa mgodi huo, Edward Heruman alisema bado hawajaanza kufuatilia suala hilo kwani kwa sasa wanaendelea kupamba na ugonjwa wa kipindupindu kwa kuweka mazingira safi.

Alisema wamekuwa wakiwatembelea mama lishe wanaozunguka mgodi huo mara kwa mara na kuwaelimisha juu ya utunzaji wa mazingira.

Miongoni mwa wachimbaji wadogo Ayub Williamu alilieleza Nipashe kuwa suala la usafi na kujikinga na kipindupindu wamelizingatia ipasavyo, isipokuwa uwepo wa madadapoa wanaofanya biashara haramu ya kujiuza katika maeneo hayo.

# W'biashara wa sukari Kanda ya Ziwa 'wakaidi' agizo la serikali

**Na Waandishi Wetu**

LICHA ya Serikali kuendelea kusisitiza wafanyabiashara wa sukari kushusha na kuuza bidhaa hiyo kwa bei elekezi, bado wameendelea kuuza bei juu kwa Sh.4000 hadi Sh.5,000.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti baadhi ya wananchi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa walisema sukari ya bei elekezi imekuwa ikipatikana kwa nadra katika baadhi ya maduka ambako wakati mwingine wakienda kuuliza wanapewa majibu kwamba imeisha.

Mkazi wa Luchelele, Dotto Hussein alisema kutokana na hali hiyo yeye na familia yake wameondoa ratiba ya chai ili kupunguza matumizi na kuendelea na mlo wa mchana na jioni pekee.

"Hiyo Sh.4500 tu nanunua sukari ambayo hata wiki haitoshi kwanini nisinunue mchele na mafuta familia ile chakula cha mchana moja kwa moja maana kwa hali hii naona hata bei elekezi wamegoma kutekeleza," alisema Hussein.

Mmoja wa wafanyabiashara kutoka eneo la Uhuru mkoani Mwanza, Ezekia Stephan alisema kwa bei anayonunulia mzingo hawezi kuuza kwa bei elekezi, huku akiiomba serikali kama ina nia ya dhati isimamie wasambazaji wakuu wa bidhaa hiyo ili wauze kwa uadilifu.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi alionesha kusikitishwa na baadhi ya wafanyabiashara hao kutokuwa waungwana kwa kuendelea kuwaminya wananchi na kusababisha baadhi yao kushindwa kufanya shughuli zao.

Hivyo, aliagiza kila mfanyabiashara anayeuza sukari kuhakikisha anabandika karatasi ya bei elekezi ya sukari mbele ya duka lake, ili pindi watakapoanza msako wa kuwabaini walanguzi wa bei ya bidhaa hiyo.

Wakati huohuo, mkoani Shinyanga kuadimika kwa sukari kumeilazimisha serikali kuwa na nia ya kuanzisha kiwanda kitakachozalisha bidhaa hiyo, sambamba na kilimo cha miwa.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Christina Mndeme, wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa RCC ambapo pamoja na mambo mengine aliwaagiza wataalam wa kilimo kufanya uchunguzi wa udongo unaoruhusu kilimo cha miwa.

"Pimeni udongo kwenye mabonde yaliyotengwa kwaajili ya kilimo cha umwagiliaji tuone kama yanafaa kwa kilimo cha miwa, ili baadae mkoa uje uanzishe kiwanda cha sukari na kukabiliana na tatizo la upungufu huu tunaokabiliana nao," alisema Mndeme.

Alisema mkoa huo una jumla ya hekta 3,155 ambazo zimetengwa kwa kilimo cha umwagiliaji, hivyo kuagiza uchunguzi ufanyike mapema iwezekanavyo ili zao hilo lianze kulimwa mkoani humo na hata kuanzisha pia Kiwanda cha Sukari (Shinyanga Sugar).

Alisema haiwezekani tatizo hilo la upungufu wa sukari liendelee kuwa kero, hivyo ni lazima watafute ufumbuzi wake mapema.

"Bado tunakabiliwa na tatizo la upungufu wa sukari huku wafanyabiashara wakiendelea kuficha bidhaa hiyo na wengine kuuza kinyume na bei elekezi ya Serikali ambayo ni Sh.2,800 na kuwaumiza wananchi kwa kuuza Sh.3,000 hadi Sh.5,000. Lazima tutafute ufumbuzi wake,"alisema Mndeme.

Kadhalika, aliwaagiza pia wakuu wa wilaya mkoani humo kutumia mbinu zote pamoja na vyombo walivyonavyo, kuwasaka wafanyabiashara ambao bado wanaendelea kuficha sukari, pamoja kuuza kinyume na bei elekezi ya Serikali na kuwachukulia hatua ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

Imeandaliwa na Vitus Audax (Mwanza) Marco Maduhu (Shinyanga)



Katibu wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA), Kanda ya Ziwa, Hashim Ramadhan, akitoa elimu kwa wakazi wa Kayenze, wilayani Ilemela, jijini Mwanza, kuhusu madhara yatokanayo na ukatili wa kijinsia, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA: Simu zaongeza kasi matumizi intaneti

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema simu za mkononi zimeongeza idadi ya watumiaji wa intenet nchini, hivyo kurahisisha na kuharakisha huduma za kiuchumi na maendeleo nchini.

Aidha, imesema watumiaji wa vifaa vilivyosimikwa na havitumii waya kama simu, laptop, tablet ni 61,645 huku wanaotumia vilivyosimikwa na vinatumia waya kama migahawa ya intenet ni 8,315.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Mwanza na Ofisa Mkuu wa Mawasiliano wa TCRA, Semu Mwakyanjala, wakati wa mahojiano maalum pembezoni mwa mkutano huo.

Alisema uwepo wa simu janja kwenye soko la simu nchini umewezesha watumiaji wengi wa mtandao kutumia simu kuzifikia huduma za mtandao wa Intaneti kwa urahisi zaidi.

Kwa mujibu wa Mwakyanjala, idadi kubwa ya watumiaji wa mtandao wa intaneti nchini hutumia huduma hizo kupitia simu za mkononi na vifaa vingine vya mawasiliano kwa mujibu wa takwimu za sekta ya mawasiliano zilizotolewa hivi karibuni na mamlaka hiyo.

Alibainisha kuwa jumla ya watumiaji wa Intaneti nchini hadi Disemba 2023 ni watumiaji 35,885,592 sawa na ongezeko la asilimia 4.1 ukilinganisha na watumiaji 34,812,739 waliokuwa wakitumia huduma hizo Oktoba mwaka jana.

Kuhusu ongezeko la watumiaji wa huduma za intaneti kwa mwaka, alisema kuwa kumekuwa na ongezeko la wastani wa asilimia 9.78 kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

"Pia, watumiaji wa intaneti wamekuwa wakiongezeka kwa mfano mwaka 2019 tulikuwa na watumiaji 25,794,560 pekee, lakini hivi leo tunazungumzia ongezeko la watumiaji wa intaneti lililofikia watu milioni 35.8," aliongeza.

Akizungumzia namna mtandao wa Intaneti ulivyorahisisha ufanyaji kazi wa shughuli mbalimbali za kiuchumi, Ofisa Mawasiliano wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Mohamed Choum alisema matumizi ya Intaneti yamekuwa yenye manufaa kwa wananchi wengi, kiasi cha kuwezesha ongezeko la watumiaji.

"Mtandao wa Intaneti umekuwa sababu wa kuziunganisha jamii, hii nadhani ndiyo sababu watumiaji wamekuwa wakiongezeka kwa kila mmoja angependa kuwamo kwenye jamii iliyounganishwa na mtandao kwa kutumia simu," alibainisha.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) huchapisha taarifa za mwenendo wa sekta ya mawasiliano kila robo ya mwaka wa fedha, ili kuhakikisha wadau wa sekta ya mawasiliano wanapata taarifa sahihi za sekta zikiwemo taarifa za ubora wa huduma za mawasiliano.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI 10 WA EPL WALIOUZWA MAPEMA UK. 12-13



# SON AMTAJA BABA SABABU KUTOKUOA HADI ASTAAFU SOKA

**LONDON,** England

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min ameelezea kwa nini hataoa hadi astaafu kucheza soka, akisema kwamba siku zote atatoa upendeleo wa kwanza kwa soka lake kuliko kitu kingine chochote.

Fowadi huyo, ambaye aliwahi kuzichezea Hamburger SV na Bayer Leverkusen kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, anachukuliwa kuwa mmoja wa mawinga bora zaidi katika soka la dunia.

Katika maisha yake yote ya soka, amefunga mabao 267 na asisti 120 katika mechi 716 kwa klabu na nchi kwa pamoja.

Son mara nyingi huitwa 'David Beckham wa Asia', kwa sababu ya soko lake na sifa ambayo inapita zaidi ya mpira wa miguu.

Ameifanya Tottenham kuwa kundi la mashabiki wa Korea, ambao mara nyingi huonekana nje ya uwanja wao wa mazoezi.

Hata hivyo, winga huyo nyota hana mpango wa kutafuta mpenzi na kutulia, akirejea wosia aliopewa na baba yake, Son Woong-jung.

Baba yake alikuwa mchezaji wa zamani wa soka ambaye alifika kiwango cha juu nchini Korea Kusini na amekuwa na jukumu kubwa katika kuunda haiba yake na maisha yake ya soka hadi sasa.

Wiki iliyopita Son alikuwa kwenye kikao cha soka cha wasichana wote wenye ulemavu katika Shule ya Vale kilichoandaliwa na Tottenham Hotspur Foundation kusherehekea siku ya Kimataifa ya Wanawake.

Akizungumzia jinsi anavyotaka kujitolea bila kuyumbayumba katika soka wakati yuko kwenye kilele cha uwezo wake, alisema, "Baba yangu alisema hivi na mimi nakubali pia.

"Unapooa, namba moja itakuwa familia, mke na watoto, na kisha mpira wa miguu. Nataka kuhakikisha kwamba wakati ninacheza katika kiwango cha juu, mpira wa miguu unaweza kuwa namba moja. Hujui ni muda gani unaweza kucheza kwenye kiwango cha juu. Unapostaafu, au unapokuwa na miaka 33 au 34, bado unaweza kuwa na maisha marefu na familia yako."

Son amewahi kuhusishwa kimapenzi na wanamuziki wa pop kutoka Korea, Bang Minah na Yoo So-young, lakini kwa sasa bado hawajaunganishwa.

Son aliwashukuru mashabiki, akitoa mfano wa Cristiano Ronaldo, akieleza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii katika mahojiano hayo.

Son alizungumza kwa uwazi kuhusu safari yake ya kucheza soka alipokuwa akikua, na kufafanua michakato yake ya mawazo kila alipoingia uwanjani.

Fowadi huyo wa Korea aliwashukuru mashabiki wake wote na kusema kwamba anatamani kulipa imani yao kwake kila mara anapoingia uwanjani.

"Nataka tu kuhakikisha ninawafurahisha kila mtu kwa kucheza katika kiwango cha juu... kwa muda niwezavyo, kuwalipa. Hili ni muhimu sana kwangu," alisema.

Son aliendelea kumtaja Ronaldo kama ndio mtu anayemfuatilia zaidi kwa kipaji chake.

"Ndiye ninayemfuatilia zaidi, Cristiano Ronaldo, ambaye anafanya kazi zaidi ya kipaji alichonacho. Ninaona wachezaji wengi ambao hawana akili, wanaofikiria kipaji pekee kinatosha. Lakini sivyo," alisema.

## ISIKUPITE

HARRY Kane amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick nne katika msimu wake wa kwanza wa Bundesliga, hii ni baada ya juzi kufunga mabao matatu wakati Bayern Munich ikiichapa Mainz 8-1. Kwa sasa nahodha huyo wa England amefikisha mabao 30 katika mechi 25 za Bundesliga.



# WACHEZAJI 10 WA EPL WALIOUZWA MAPEMA

**LONDON,** England

LIGI Kuu England (EPL), inayosifika kwa kasi na ushindani mkali, imekuwa hatua ambapo vipaji vingi vya soka vimestawi kwa miaka mingi. Hata hivyo, katikati ya mng'aro, kumekuwa na matukio ambapo klabu ziliachana na wachezaji kabla ya wakati, na kushuhudia tu wakichanua na kuwa nyota mahali pengine.

**Katika makala haya, tunaangazia safari za wachezaji 10 wa Ligi Kuu England ambao waliuzwa mapema mno, na kuwaacha mashabiki na wadadisi wakitafakari nini kilitokea.**

### #1. Salah (Chelsea kwenda Roma)

Muda wa Mohamed Salah katika klabu ya Chelsea kuanzia mwaka 2014 hadi 2016, ulitatizwa na muda mfupi wa kucheza na akapata shida kuzoea hali ya Ligi Kuu England. Hata hivyo, uhamisho wake wa baadaye wa AS Roma uliboresha kazi yake, akionesha kasi yake, umaliziaji mzuri na uwezo wake wa kufunga mabao.

Uchezaji wa kipekee wa Salah kule Serie A hatimaye ulimfanya kuhamia Liverpool, ambako alibadilika na kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani, akitwaa tuzo nyingi binafsi na kuisaidia Liverpool kupata mataji ya kifahari, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu.

### #2. Xabi Alonso (Liverpool kwenda Real Madrid)

Kutokana na kipindi cha mafanikio akiwa Liverpool, ambapo alikuwa kiungo mahiri aliyependwa na mashabiki wa Anfield, Xabi Alonso, alihamia Real Madrid mwaka 2009 kwa kustaajabisha.

Upigaji pasi wa kiungo huyo wa Hispania, uwezo wake wa kuona, na akili zake ziliisaidia sana Real Madrid, ikiwa ni pamoja kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kuondoka kwa Alonso kuliacha pengo katika safu ya kiungo ya Liverpool, na mchango wake kwa Real Madrid ulidhihirisha thamani yake kama mchezaji aliyeuzwa mapema mno.

### #3. Kevin De Bruyne (Chelsea kwenda Wolfsburg)

Muda wa Kevin De Bruyne akiwa Chelsea ulikuwa mfupi, ukiwa na nafasi chache za kuonesha kipaji chake uwanjani. Lakini kuhamia Wolfsburg mnamo 2014 kulikuja kuwa hatua ya mabadiliko katika taaluma yake. De Bruyne alinawiri katika Bundesliga, akionesha ubunifu wake, pasi za uhakika na jicho la bao.

Uchezaji wake ulimfanya ahamishwe kwa kasi hadi Manchester City, ambako alijidhihirisha kuwa mmoja wa viungo bora katika Ligi Kuu England, akishinda mataji mengi ya Ligi Kuu na mengine ya ndani.

### #4. Gerard Pique (Manchester United kwenda Barcelona)

Kuondoka kwa Gerard Pique kutoka Manchester United kwenda Barcelona mwaka 2008, kuliibua hisia, lakini ilionekana kuwa jambo la kushangaza kwa wababe hao wa Katalunya.

Ingawa alishinda mataji machache akiwa na Manchester United, ambayo yalijumuisha taji la Ligi Kuu, ilikuwa ni Barcelona ambapo Pique alichanua na kuwa mmoja wa walinzi bora zaidi wa kati duniani, na kuunda ushirikiano wa kutisha na wachezaji kama Carles Puyol na Javier Mascherano.

Uwezo wake wa kuusoma mchezo, mtindo wa uchezaji maridadi, na sifa za uongozi zilikuwa muhimu katika utawala wa Barcelona ndani na Ulaya, na hivyo kufanya kuondoka kwake Manchester United kutokuwa wa kujutia kwake.



SALAH

### #5. Juan Mata (Chelsea kwenda Manchester United)

Uhamisho wa Juan Mata kutoka Chelsea kwenda Manchester United mnamo 2014 ulikuja kuwashangaza wengi, ikizingatiwa jukumu lake kuu pale Stamford Bridge. Ubunifu wa Mata, ustadi wa kiufundi na jicho kwa bao lilimfanya apendwe na mashabiki wa Chelsea, lakini kuondoka kwake kulifungua njia kwa ukurasa mpya Old Trafford.

Licha ya ugumu wa awali kuiga kiwango chake cha Chelsea, Mata alikuwa mchezaji thabiti wa Manchester United, akionesha akili yake uwanjani na kuchangia mabao na pasi za mabao muhimu kwa miaka mingi.

### #6. Serge Gnabry (Arsenal kwenda Bremen)

Kuondoka kwa Serge Gnabry kutoka Arsenal kwenda Werder Bremen mwaka wa 2016 kuliibua hisia, hasa ikizingatiwa uwezo wake na mwanga wa kipaji wakati alipokuwa Kaskazini mwa London. Lakini ilikuwa huko Bayern Munich ambapo Gnabry alijitangaza kweli kwenye hatua ya kimataifa.

Kasi yake ya kusisimua, uwezo wa kuchezea chenga, na umaliziaji wake uliifanya Bayern kuwa katika utukufu wa ndani na Ulaya, na hivyo kuimarisha hadhi yake ya kuwa mmoja wa mawinga wanaosisimua zaidi katika soka la dunia. Uamuzi wa Arsenal kumwachia Gnabry bila kutumia uwezo wake kikamilifu ni kosa la kujutia.

### #7. Carlos Tevez (Manchester City kwenda Juventus)

Wakati wa Carlos Tevez akiwa Manchester City ulijaa wakati wa uzuri na mabishano. Lakini kuondoka kwake kwenda Juventus mnamo 2013 kulikuja kama mshangao kwa mashabiki wengi wa Ligi Kuu. Uimara wa Tevez, kiwango cha kazi, na ustadi wa kupachika mabao kulimfanya apendwe na mashabiki wa Manchester City, na kutokuwapo kwake kuliacha pengo kubwa katika safu ya ushambuliaji ya timu hiyo.

Akiwa Juventus, Tevez aliendelea kufanya vema, akicheza nafasi muhimu katika ushindi wao wa Serie A na kujiimarisha kama mmoja wa washambuliaji wa kuogopwa sana katika soka la Ulaya.

### #8.Cole Palmer (Manchester City kwenda Chelsea)

Kuondoka kwa Cole Palmer kutoka Manchester City kwenda Chelsea mnamo 2023 kulizua sintofahamu, haswa kutokana na uwezo wake na uchezaji wake mzuri katika maandalizi ya vijana wa City.

Wakati uhamisho wa Palmer kwenda Chelsea ukiwa bado katika hatua zake za awali, kuondoka kwake Manchester City kukainyima klabu hiyo mchezaji mwenye kipaji ambaye angeweza kuleta matokeo kwenye kikosi cha kwanza. Ni wakati tu ndio utakaoamua kama City watapuuza uamuzi wa kumruhusu Palmer kuondoka, lakini kuondoka kwake bila shaka kunazua maswali kuhusu mkakati wa maendeleo ya vijana wa klabu hiyo.

### #9. David Beckham (Manchester United kwenda Real Madrid)

Kuondoka kwa David Beckham kutoka Manchester United kwenda Real Madrid mwaka 2003, kulileta mshtuko katika ulimwengu wa soka. Beckham, anayejulikana kwa krosi zake, ustadi wake na sura nzuri, alifurahia mafanikio makubwa akiwa na Manchester United, akishinda mataji mengi ya Ligi Kuu England na kuwa nahodha wa timu hiyo.

Hata hivyo, uhamisho wake wa kwenda Real Madrid ulimpandisha hadhi zaidi kama nyota wa kimataifa, akicheza pamoja na magwiji kama Zinedine Zidane na Ronaldo. Kuondoka kwa Beckham kutoka Manchester United kuliashiria mwisho wa enzi, na kuwaacha mashabiki na wasiwasi kwa haiba yake isiyo na kifani na uzuri wa uwanjani.

### #10. Raheem Sterling (Liverpool kwenda Manchester City)

Kuondoka kwa Raheem Sterling kutoka Liverpool kwenda Manchester City mwaka 2015, kulikumbwa na hisia tofauti kutoka kwa mashabiki wa klabu zote mbili. Wakati uwezo wa Sterling ulionekana wazi wakati akiwa Anfield, uhamisho wake wa kwenda Manchester City ulimpa jukwaa la kutimiza ahadi yake.

Kasi ya Sterling, ustadi wa kucheza chenga na uwezo wa kufunga mabao umekuwa muhimu katika utawala wa ndani wa Manchester City, na kuisaidia klabu hiyo kupata mataji mengi ya ligi.

Kuondoka kwake kutoka Liverpool kuliacha pengo katika safu yao ya ushambuliaji, na kuangazia athari za kumuuza mchezaji haraka sana.

Matukio ya wachezaji hawa 10 wa Ligi Kuu England yanadhihirisha uwiano wa klabu lazima utokee kati ya kukuza vipaji vya vijana na kufanya maamuzi ya uhamisho wa busara. Ingawa mtazamo wa nyuma ni 20/20, mifano hii hutumika kama ukumbusho kwamba subira na mtazamo wa mbele ni muhimu katika hali inayoendelea ya uhamisho wa soka.

Wakati klabu zikiendelea kutafuta vipaji vikubwa vijavyo, lazima vijifunze kutokana na makosa yaliyopita na kuepuka kutengana na wachezaji ambao wana uwezo wa kung'ara kwenye hatua kubwa zaidi za soka duniani.

## Nukuu

"Bwana Ancelotti alikuwa wa kushangaza sana. Hapo mwanzo nilifikiri alikuwa zaidi ya mtu mgumu, zaidi ... aina ya kiburi, na ilikuwa kinyume chake. Yeye ni kama dubu mkubwa, naweza kusema. Yeye mtu nyeti sana. Alizungumza nasi kila siku. Si tu na mimi bali na wachezaji wote. Alifurahi nasi. Natamani kila mchezaji apate nafasi ya kufanya naye kazi kwa sababu ni mtu mzuri sana. Ninatamani pia kufanya kazi naye siku moja tena," **Mshambuliaji wa Al Nassr, Cristiano Ronaldo**



"Makosa ni sehemu ya soka, ndivyo unavyoyachukulia, hasa kwa walinda mlango ambayo pengine ndiyo nafasi ngumu zaidi. Sishangai kwa sababu timu nzima na uwanja mzima ulikuwa nyuma yake. Amepata heshima hiyo na kupongezwa. Tulitamani sana kushinda kwa ajili yake," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, baada ya kipa Aaron Ramsdale kufanya makosa na kuiruhusu Brentford kusawazisha kwenye mechi ya Ligi Kuu juzi, kabla ya Kai Havertz kufunga la ushindi na kuwa 2-1.**



"Mbappe, samahani, samahani. Wote ni wazuri. Hakuna jibu baya au lisilo sahihi hapa, lakini ... Mbappe jamani. Ningelipa kila siku kumtazama akifanya mazoezi achilia mbali kucheza mechi, kwa sababu anatengeneza mambo peke yake. Ninaweza kumpa mpira kwenye beki ya kushoto na anaweza kufunga. Naweza kumpa mpira popote pale uwanjani na anaweza kutengeneza kitu. Hao wengine wawili sio sana. Ni wazuri sana, usinielewe vibaya. Lakini Mbappe ana kitu tofauti ambacho kingenifanya niketi usiku," **Beki wa zamani wa Man United na mchambuzi wa soka, Rio Ferdinand akimtaja mchezaji anayevutiwa naye zadi kati ya Kylian Mbappe, Erling Haaland na Harry Kane.**





# REKODI, TAKWIMU LIGI KUU BARA KATIKA NAMBA

Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum, akipongezwa na wenzake, katika moja ya mabao aliyoyafunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara imeingia kwenye raundi ya 20, ambapo baadhi ya timu zimebakisha michezo 10 tu kuweza kuhitimisha msimu huu, huku zingine zikiendelea kumalizia viporo.

**Inaonekana kabisa kuwa ndani ya ligi hiyo kuna vita tatu inayopiganwa, ya kwanza ni timu zinazosaka ubingwa, zinazopigania nafasi nne za juu na nyingine ni zile zinazopigania uhai wa kubaki Ligi Kuu msimu ujao.**

Timu za Yanga, Simba na Azam zimejikatia kipande chao zikionekana ndizo pekee zinazopigania ubingwa.

Hata hivyo, Yanga ndiyo inaonekana kama imepania zaidi kuutwaa ubingwa mara ya tatu mfululizo, huku zilizobaki zikiwa na mwendo wa kupanda na kushuka.

Wachezaji na timu zote 16 zinazoshiriki nao wanajiwekea rekodi mbalimbali na kuifanya ligi kuwa na mvuto.

Katika makala haya tumekusanya rekodi na takwimu zilizowekwa na timu, pamoja na wachezaji wa Ligi Kuu mpaka kufikia raundi ya 20.

**46#.** Hizi ni pointi zinazomilikiwa na vinara wa Ligi Kuu mpaka sasa Yanga ambayo inausaka ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo ikiwa kileleni.

**45#.** Idadi ya mabao iliyofunga Azam FC kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa ambayo inausaka ubingwa ili iutwae kwa mara ya kwanza tangu 2013/14.

**44#.** Azam FC inayoshika nafasi ya pili kwenye ligi, ina idadi hii ya pointi mpaka sasa

**42#.** Vinara wa Ligi Kuu, Yanga wamefunga idadi hii ya mabao mpaka sasa dhidi yale ya Azam FC, pungufu ya mabao matatu, kabla ya mechi ya leo dhidi ya Ihefu FC.

**39#.** Baada ya kushinda mechi yake ya juzi mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Simba inafikisha idadi hii ya pointi.

**35#.** Ni idadi ya mabao ya kufunga ya Simba, ikiwa ni timu ya tatu kufunga mabao mengi kwenye ligi, Azam FC ikiongoza ikifuatiwa na Yanga.

**27#.** Hizi ni pointi zinazomilikiwa na timu mbili ambazo juzi zimepata vipigo. Coastal Union baada ya kufungwa mabao 2-1 dhidi ya Simba, imesalia nafasi ya nne kwa idadi hiyo ya pointi, huku Prisons ambayo ilifungwa 2-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, ina idadi kama hiyo ya pointi, ikishika nafasi ya tano ya msimamo wa ligi hiyo.

**23#.** Idadi hii ya pointi inamilikiwa na timu nne, ambazo ni Namungo iliyo nafasi ya saba, Ihefu kwenye nafasi ya nane, Dodoma Jiji nafasi ya tisa na Kagera Sugar nafasi ya 10. Kinazozitofautisha ni idadi ya mabao ya kufunga na kufungwa.

**21#.** Singida Fountain Gate, Mashujaa FC, Tabora United, Geita Gold, zote hizo zina idadi hiyo ya pointi kila moja.

Singida imekaa juu ya timu hizo ikiwa nafasi ya 11 kwa idadi kubwa ya mabao, Mashujaa ikiwa ya 12, Tabora United nafasi ya 13 na Geita Gold ipo nafasi ya 14.

**20#.** Ligi Kuu Tanzania Bara imefika kwenye raundi hii, ambapo robo tatu ya timu zote zimecheza idadi hii ya mechi.

**19#.** Timu ya JKT Tanzania inayoshika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, imecheza idadi hii ya mechi, lakini pia ina idadi kama hii ya pointi.

**17#.** Ni idadi ya mabao ambayo Simba imeruhusu kwenye nyavu zake mpaka sasa kwenye ligi, ikishika nafasi ya tatu kwa kuruhusu idadi ndogo ya mabao, baada ya Yanga, Azam na Coastal Union ambazo zote zimeruhsu idadi sawa ya mabao.

**15#.** Pamoja na kushinda mabao 2-1 juzi dhidi ya Prisons, timu ya Mtibwa Sugar bado inashika mkia, ikiwa na idadi hii ya pointi, ikicheza michezo 19.

**12#.** Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum, amefunga idadi hii ya mabao akiwa kinara wa mabao mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

**11#.** Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki wa Yanga ana idadi hii ya mabao mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**10#.** KMC ndiyo timu iliyotoa sare nyingi zaidi kwenye ligi mpaka sasa, ikiwa imefanya hivyo mara10.

**9#.** Ni idadi ya mechi zilizopotezwa na timu za Mashujaa FC na Geita Gold kwenye ligi mpaka kufikia raundi ya 20.

**8#.** Namba hii inasimama kama idadi ya mabao ambayo wachezaji, Maxi Nzengeli wa Yanga, Marouf Tchakei wa Ihefu FC, Jean Baleke aliyekuwa akiicheza Simba na Waziri Junior, wameyafunga kila mmoja kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**7#.** Timu za Coastal Union, Prisons, Namungo, Kagera Sugar na Tabora United zimepoteza mechi zao mara idadi hii.

**5#.** Ni idadi ya sare ambazo Azam imezipata mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikishika nafasi ya tatu kwa kuwa nazo chache zaidi, baada ya Yanga na Simba.

**3#.** Hii ni namba inayowakilisha idadi ya sare za Simba kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ikishika nafasi ya pili kwa kuwa nazo chache zaidi.

**2#.** Simba na Azam zote zimepoteza mechi mbili kila moja mpaka sasa kwenye ligi, zikiwa zinashika nafasi ya pili kwa kupoteza mechi chache zaidi mpaka sasa.

**1#.** Namba hii inaonyesha kuwa Yanga ndiyo timu iliyopoteza idadi hiyo ya mechi, ikichapwa na Ihefu FC, pia ni idadi ya sare ambayo inayo mpaka sasa, ambayo ilikuwa ni suluhu dhidi ya Kagera Sugar.

## JE, WAJUA?

Premier League

TANGU Msimu wa Ligi Kuu England 1993/94 hadi huu wa 2023/24 unaoendelea, Klabu ya Swindon ndiyo iliyoruhusu mabao mengi zaidi kwa msimu (100), ikifuatiwa na Ipswich 1994/95 (mabao 93), Derby 2007/08 (mabao 89), Fulham 2013/14 (mabao 85) na Norwich 2021/22 (mabao 84). Kwa msimu huu hadi sasa Sheffield United imesharuhusu mabao 74 katika mechi 28 huku Burnley ikiruhusu 60 kwenye mechi 27.



# Watu 33, 000 hufariki dunia kwa kuvuta moshi wa mkaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAKWIMU zinaonyesha kuwa hapa nchini watu 33,000 wanafariki dunia kila mwaka kwa kuvuta moshi na chembechembe zinazotokana na mkaa na kuni.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman aliyasema hayo juzi mkoani hapa wakati wa kongamano la wanawake la kugawa mitaji na vitendea kazi vya nishati safi ya kupikia yakiwamo majiko ya gesi ya Oryx.

Alisema kwa zaidi ya miaka 15, upatikanaji wa suluhisho la kupikia kwa nishati safi umekuwa ukijadiliwa na kupangwa, lakini sasa imekuwa mada ya muhimu, chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Araman alisema katika kuunga mkono ajenda ya nishati safi ya kupikia Oryx Tanzania imeweka mkakati maalum wa kukuza matumizi ya nishati hiyo. Alisema hadi sasa mitungi ya gesi na majiko ya zaidi ya 24,000 yenye thamani ya Sh.bilioni mbili imetolewa kwa makundi mbalimbali ya wanawake.

Pia alisema kupika kwa gesi kunasaidia katika kulinda mazingira kwani huzuia ukataji miti, hivyo husaidia kulinda mazingira. Kuhusu hali za maisha, alisema kupika kwa kutumia gesi ya Oryx huzuia wanawake kutumia saa nyingi kwa ajili ya kukusanya kuni kutoka msituni, huku pia akielezea namna ambavyo gesi inavyosaidia wanawake kukabiliwa na hatari katika misitu ya wanyamapori pamoja na kukutana na majanga mengine.

Pia, aliishukuru serikali kwa kuwaunga mkono katika mipango yao ya nishati safi kwa kuhakikisha matumizi ya gesi ya Oryx jijini Dodoma na Tanzania kwa ujumla.



Makamu wa Rais Dk Philip Mpango (kushoto) akimsikiliza Mkurugenzi wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman wakati alipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye kongamano la wanawake la kugawa mitaji na vitendeakazi vya nishati ya kupikia lililofanyika Jijini Dodoma mwisho wa wiki kwa kuandaliwa na Wizara ya Nishati. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Dk. Biteko: Samia hataki kuona wawekezaji wakipata misukosuko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema Rais Samia Suluhu Hassan hataki kuona wafanyabiashara wakipata misukosuko kwenye uwekezaji.

Aidha, amesema maeneo mengi nchini bado yanahitaji uwekezaji wa malazi, ikiwamo Dodoma kutokana na wageni kukosa malazi hasa kunapokuwa na mikutano mikubwa.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Hoteli ya Rafiki jijini hapa, kusema nia ya Rais Samia ni kuhakikisha kwamba sekta binafsi inakuwa kwa mchango mkubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

"Nitoe wito kwa watumishi wa serikali kwamba tunaowajibu wa kusaidia sekta binafsi, ifike mahali tuone aibu kama wewe ni Ofisa wa Tanesco, una wajibu wa kumuunganisha mfanyabiashara na umeme ambao mwisho wa siku ataulipia kwa ajili ya mapato ya nchi."

"Ona aibu kumwambia njoo kesho wakati kazi hiyo ungeifanya leo, wale wanaotoa vibali vya ujenzi tunaona raha kuwa na urasimu na kuonesha tuna madaraka ya kumfanya mtu njoo kesho wakati jambo lenyewe nila kunyanyuka mara moja kwenda kumhudumia mlipakodi huyu ili aweze kuwekeza kupata kodi zaidi, ikulipe mshahara wewe mwenyewe unaleta urasimu mahali pa kazi,"alisema.

Kuhusu upungufu wa malazi, Naibu Waziri Mkuu huyo alisema pamoja na jitihada zilizofanywa za kukuza sekta ya utalii bado kuna upungufu wa maeneo ya malazi ya kuwaomba wawekezaji kuliangalia suala hilo.

# TANESCO yapewa angalizo uuzaji umeme nje ya nchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAJUMBE wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Singida imetoa tahadhari kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), juu ya mpango wake wa kutaka kuuza umeme nje ya nchi, ikisema isije ikaingiza nchi kwenye matatizo ya kushtakiwa na kudaiwa mabilioni ya fedha.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na wajumbe hao walipofanya kikao kiliongozwa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba ambaye kwa sasa amehamishiwa katika Mkoa wa Iringa.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Katibu Mkuu Msaidizi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi Kati, Mchungaji Edward Gyunda, alisema mpango wa kuuza umeme nje ni mzuri lakini kuna mashaka endapo umeme huo utakuwa unakatikatika kama ilivyo sasa chinini, hali ambayo inaweza kusababisha nchi kushtakiwa.

Alisema baadhi ya nchi umeme unapokatika kwa kuwa unaharibu vifaa vya ndani mwananchi au wananchi wanachukua hatua ya kushtaki shirika linalozalisha umeme na kudai fidia ya mamilioni ya fedha, jambo ambalo litayumbisha nchi mpango huo wa kuuza umeme nje utakapoanza kutekelezwa.

"Naingiwa hofu huu umeme ambao unakatika nchini kweli utaweza kuuzwa hadi nje? ,tuwe na tahadhari tusije tutakuta Tanesco wanaingia katika kesi maana kuna nchi umeme ukikatika wanashtaki sababu unaharibu vifaa," alisema.

Mhandisi Mkuu wa Tanesco Mkoa wa Singida, Channy Damas, aliwatoa hofu wajumbe wa RCC kwamba bwawa hilo litazalisha umeme wa kutosha ambao utasaidia kupunguza tatizo la kukatika kwa umeme nchini.

Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, alisema Tanesco wanapaswa kuweka utaratibu mzuri ili wananchi wajulishwe gharama halisi za kuunganishiwa umeme kwani kumekuwa na sintofahamu baadhi wanaingiziwa kwa Sh.27,000 na wengine Sh.300,000 hadi 500,000.

Alisema Tanesco pia wanapaswa kuweka kipaumbele kupeleka huduma ya umeme kwenye taasisi za umma kama shule na hospitali ambazo zimejengwa hivi sasa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni,Jumanne Mlagaza, alisema Tanesco wanapotekeleza miradi ya umeme wanaacha madeni mengi kwa wafanyakazi wao bila kuwalipa jambo ambalo halileti taswira nzuri.



# Wodi ya wanawake yapokea msaada vifaa tiba vya mil.6/-

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Kampuni ya Mafuta ya Puma Tanzania, imewashika mkono kinamama wilayani Kigamboni kwa kutoa vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya hiyo.

Vifaa tiba hivyo ni pamoja na viti mwendo na vifaa vya kupima presha vyenye thamani ya Sh. milioni 6.5 kwa wodi ya wanawake katika hospitali hiyo iliyopo Kibugumo, Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Fatma Abdallah akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa tiba hivyo, alisema Puma Energy inaamini vifaa vilivyokabidhiwa vitaleta ahueni kwa jamii.

"Machi 8, ya kila mwaka imekuwa ikiadhimishwa Siku ya Wanawake Duniani, tumeona tusikae nyuma, hivyo tumejumuika na wenzetu kuadhimisha siku hii kitofauti. Tumeona tuguse jamii na jamii yenyewe ni inayotuzunguka.

"Puma tumekuja kukabidhii vifaa tiba katika wodi ya wanawake katika Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni, tumejitahidi kukusanya vifaa tiba kadhaa vyenye thamani ya Sh. milioni 6.5. Tunavyo vifaa tiba mbalimbali kama viti mwendo na mashine za kupima presha, tunaamini vitasaidia katika wodi ya wanawake," alisema.

Aliongeza: "Tunafahamu wodi ya kinamama ni eneo lenye changamoto nyingi na wagonjwa wengi. Hivyo kunahitajika uangalizi tofauti, siyo kwamba tunajipendelea sisi wanawake lakini wodi ya wanawake inahitaji uangalizi wa tofauti kidogo".

Alisema Puma kuna wanawake zaidi ya 48 na hatua kubwa imepigwa kuanzia mwaka 2023 kwani wakati anaingia kulikuwa na wafanyakazi wanawake asilimia tisa lakini hivi sasa imefika asilimia 16, huku akisisitiza wanawake wengi wameingizwa kwenye uongozi.

Hata hivyo alisema wanaendelea kutengeneza mazingira ya kuwawezesha, kuwathaminisha na kuwaleta pamoja wanawake ili waweze kuleta maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Kaimu Mganga Mfawidhi Matroni, Eva Sambaya aliwashukuru Puma Energy kwa kuwapatia vifaa hivyo akisema imeonyesha kuwathamini na kuwajali.

"Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani Puma mmeona haja ya kuja kwetu na kutushika mkono, vifaa hivi kwetu vitasaidia katika kutoa huduma katika wodi ya wanawake." Alisema.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Dk.Lucas Ngamtwa alitoa shukrani kwa kampuni ya Puma kwa namna ambavyo wameguswa na kuamua kuwashika mkono katika hospitali hiyo.



Katibu Mkuu wa Umoja wa wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Jokate Mwegelo (katikati) akiwa ameongozana na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (kulia) alipowasili katika ofisi ya CCM Mkoa wa Mbeya jana kwa ajili ya ziara ya kikazi. **PICHA:NEBART MSOKWA.**

# CCM yaonya wataokwamisha wanawake uchaguzi wa mitaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kimesema kitachukulia hatua kali dhidi ya watu watakaobainika kukwamisha wanawake wenye sifa za uongozi watakaojitokeza kuwania uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela aliyasema hayo juzi alipokuwa anafunga Mkutano wa Baraza la Vijana wa chama hicho (UVCCM) Mkoa wa Mbeya ulioambatana na mafunzo ya uongozi na ujasiriamali.

Aliwataka wajumbe wa kamati za siasa za wilaya kuwasaidia wanawake watakaotia nia kwenye nafasi hizo ili washinde na kuongeza idadi ya wanawake kwenye serikali.

Alisema wanawake wakishinda kwenye nafasi hizo itakuwa rahisi kutatua baadhi ya matatizo yakiwemo yanayohusu watoto na huduma mbalimbali za kijamii ambazo asilimia kubwa wao ndio wanazitumia zaidi kuliko wanaume.

"Lakini pia nadhani wote tunajua 'integrity' (uadilifu) wa watoto wa kike, kwahiyo sisi kama chama tutahakikisha mtoto wa kike yeyote atakayetia nia, akiwa na sifa tunamsaidia apite ili kama ni kushindwa akashindwe kwenye sanduku la kura," alisema Mwaselela.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kuepuka kuwabagua wagombea watakaotia nia kwenye uchaguzi huo kwa namna yoyote ikiwemo jinsi zao, huku akisisitiza kuwa ubaguzi huo hautavumiliwa na viongozi wa chama.

Alisema chama hicho kitawashughulikia watu wote ambao watawanyanyasa ama kuwabagua wanawake watakaojitokeza kwenye uchaguzi huo.

Pia aliwataka vijana wa chama hicho kushirikiana na kuhakikisha wanakisaidia chama hicho kupata ushindi kwenye mitaa, vijiji na vitongoji vyote.

Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Mbeya, Yassin Ngonyani alisema wamekubaliana kuifanya ajenda ya uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kuwa ya kudumu kwenye vikao.

Alisema watafanya kazi kwa kuzingatia taratibu za uanzishwaji wa umoja huo ikiwemo kuhakikisha wanakisaidia chama hicho kupata ushindi kwenye kila uchaguzi.

"Sisi tumeshakubaliana kwamba tutahakikisha tunafanya kazi ya kukisaidia chama kama ambavyo umoja wetu unajulikana kuwa ni mkono wa kuume wa CCM," alisema Ngonyani.

Aliwaomba viongozi wa chama hicho kuendelea kuwajenga vijana wa umoja huo ili wawe warithi sahihi wa nafasi za uongozi za juu za chama hicho.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCM Wilaya ya Chunya, Maalim Goza aliwataka vijana kufanya kazi ya kuwatetea wananchi badala ya kuwa 'machawa' wa baadhi ya viongozi wa chama na serikali.

Alisema kihistoria viongozi wengi wa chama na serikali walikuwa wanatokana na umoja huo na walikuwa wanafanya kazi ya kuibua kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

# TAKUKURU: Wanawake msifumbie macho rushwa ya ngono

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WANAWAKE mkoani Njombe wametakiwa kutofumbia macho vitendo vya rushwa hasa rushwa ya ngono inayosababisha udharirishaji na kuharibu utu wa mwanamke.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Wanging'ombe, Scholastica Assey kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yanayofanyika kimkoa katika Kijiji cha Usita wilayani Wanging'ombe.

Assey aliwataka wanawake kuwa na ujasiri wa kutoa taarifa zinazohusu vitendo vya rushwa kwa kuwa suala la rushwa ni suala linalomgusa kila mtu.

"Masuala ya rushwa yanatugusa wanawake haswa rushwa ya ngono, tusikae kimya inapotokea umeombwa rushwa hata kwenye maeneo ya kazi toa taarifa haraka kupitia namba ya bure 113, suala hili linatudhalilisha sisi wanawake," alisema Assey.

Aidha pia aliwahimiza wanawake kuwa vinara wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao ili kuhakikisha hakuna ubadhirifu unaotokea ili miradi hiyo iwe na tija kwa jamii.

"Ni muhimu kwa wanawake wote kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka 2024 na uchaguzi mkuu ujao na kuzingatia kutojihusisha na vitendo vya rushwa kipindi chote cha uchaguzi," alisema Assey.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka aliwataka wanawake mkoani humo kutafuta maarifa yatakayowasaidia kuongeza kipato na kukuza uchumi kwenye familia zao.

Mtaka alisema wanawake walio kwenye vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana kuacha kukaa kwa mazoea na badala yake wafikiri namna ya kuongeza ujuzi na maarifa kwa kualika watu waliofanikiwa kwenye biashara kuwapatia elimu na uzoefu.

Alisema: "Mwanamke anauwezo mkubwa wa kumlea na kumjenga mtoto wa kike na wakiume, wanawake ni jeshi kubwa tengenezeni jeshi kubwa kwenye uchumu tumieni mikutano yenu ya wanawake kufundishana mambo ya msingi."



# Serikali yatangaza bei ya sukari mfungo wa Ramadhani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI waumini wa dini ya kiislamu wanatarajia kuanza mfungo wa mwezi wa Ramadhani, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetangaza bei elekezi ya sukari ili kuwapunguzia gharama wananchi.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari juzi wilayani Mjini Unguja, Waziri wa Wizara Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban alitaja bei ni Sh. 2,650 kwa kilo moja kwa upande wa Unguja na Sh. 2,700 kwa kilo kwa upande wa Pemba.

Alisema hatua hiyo imekuja kufuatia agizo la Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi alilolitoa hivi karibuni katika ziara yake ya kutembelea wafanyabiashara na kusikiliza changamoto zao.

Katika ziara hiyo Dk. Mwinyi aliitaka Wizara ya Biashara kutoa bei elekezi ya kuuzia sukari baada ya serikali kuondoa gharama za kodi katika bidhaa hiyo, ili kupunguza makali ya maisha hasa katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Alisema kufuatia agizo hilo Wizara ya Biashara imeelekeza wafanyabiashara wote kushusha bei ya sukari katika kipindi cha Ramadhani na kuuza kwa hiyo iliyotajwa.

Akizungumzia bei elekezi ya wauzaji wa jumla alisema bidhaa hiyo itauzwa kwa shilingi 123,000 upande wa Unguja na Shilingi 126,000 kwa upande wa Pemba ambapo waingizaji wa bidhaa hizo watauza kwa shilingi 121,000 kwa upande wa Unguja na shilingi 124,000 kwa upande wa Pemba kwa ujazo wa kilo 50.

Alisema kuwa bei hizo zimezingatia utoaji wa kodi na faida kwa kila mmoja hivyo aliwataka wafanyabiashara hao kutekeleza agizo hilo, kwamba hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakaekwenda kinyume na agizo hilo ikiwemo kufutiwa leseni ya biashara.

Aidha, aliwataka watendaji wa Tume ya Ushindani Halali ya Biashara kutekeleza wajibu wao na kuhakikisha sukari inauzwa kwa bei elekezi katika kipindi chote cha mwezi mtukufu wa Ramadhan mpaka itakapotangazwa bei nyingine.

Pia aliwataka wafanyabiashara kutopandisha bei kwa bidhaa ambazo hazijatolewa bei elekezi na kuweka unafuu kwa wananchi ili kumudu gharama za mwezi huo.

"Hiki si kipindi cha kuchuma faida nyingi za kifedha ni kipindi cha kuchuma thawabu, hivyo tuwe na mazingatio na tukumbuke kwamba tunatoa unafuu kwa wananchi wenzetu" alisema.

Kadhalika aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya na masheha kuisaidia Serikali katika kuhakikisha dhamira ya Rais Dk. Mwinyi ya kuwasaidia wananchi katika kipindi cha Ramadhani na kuhakikisha wanapata mahitaji yao kwa bei nafuu inafikiwa .

Kabla ya Serikali kutangaza bei elekezi sukari ilikuwa inauzwa Sh. 3,000 kwa kilo moja.




Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban (katikati) akishuhudia kubadilishana kwa makubaliano ya ushirikiano kati ya Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wapili kulia) kwa niaba ya Benki na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO), Dk Masoud Rashid Mohamed katika makao makuu ya Benki ya NMB jijini Dar es Salaam. Kulia ni Meneja wa Biashara za Zanzibar wa Benki ya NMB, Naima Shaame na kushoto ni Mkuu wa idara ya Kilimo wa Benki hiyo, Nsolo Mlozi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB, ZASCO zaingia makubaliano kuongeza thamani mwani Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB na Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) zimetia saini Hati ya Makubaliano (MoU) ya ushirikiano kuongezea thamani zao la kimkakati la mwani na kupanua wigo wa mchango wake katika kukuza Uchumi wa Buluu visiwani Zanzibar.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ambako Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alishuhudia Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi na Mkurugenzi Mkuu wa ZASCO, Dk. Masoud Mohammed Rashid, wakitia saini hati hiyo.

Mwani ni aina ya mimea inayoota na kukua kwenye maji chumvi (bahari) na maji baridi (mito, maziwa na mabwawa), zao ambalo hutumika kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vyakula, juisi, shampoo, sabuni, mafuta ya kupaka, jamaa ya matunda, dawa za meno, viungo vya chakula na mafuta ya nywele.

Akizungumza kabla ya kutiwa saini makubaliano hayo, Waziri Omar aliishukuru NMB kwa kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) za kuchakata Sera ya Uchumi wa Buluu. Wanaamini makubaliano hayo baina ya NMB na Zasco yanakwenda kulipa thamani zao la mwani kulipiku zao la karafuu.

"Rekodi zinaonesha kuwa bei ya mwani iliyoongezwa thamani ni kubwa kulinganisha na karafuu, hivyo kwa aina hii ya ushirikiano, mwani inakwenda kupiku thamani ya karafuu kimapato. Kama kwa muda mrefu karafuu imetupa fedha za kigeni, mwani pia inayo fursa hiyo iwapo tutawekeza vizuri hivi.

"Mwani ni zao la kimkakati na tunashukuru NMB kuungana nasi katika mkakati huu, tunaamini kwamba ushirikiano huu wa NMB na ZASCO utatusaidia katika maeneo matatu, ambayo ni kuongeza maendeleo yenye tija kwa wajasiriamali wadogo wa mwani, kupata mitaji, mikopo na ujuzi au elimu.

"Kwa sababu ingawa wanaosaini makubaliano haya ni ya NMB na ZASCO, wanufaika wakuu na wa awali si wao. NMB na ZASCO jukumu lao ni kusapoti kwanza wajasiriamali wadogo ambao ndio walengwa, ndio maana tunaliona jambo zuri linalopaswa kuungwa mkono na wadau wengine wa maendeleo

"Tunaishukuru NMB kwa ushirikiano wao, na mimi niwahakikishie kwamba SMZ kupitia wizara yangu, tunaona na kuthamini jitihada zenu zote katika maeneo mbalimbali zinazochochea uchumi wa Zanzibar na kuisaidia serikali kutekeleza mikakati yake," alisisitiza waziri huyo.

Awali, Mponzi aliipongeza SMZ chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye maono yake ya kukuza Uchumi wa Bluu, yaliivutia NMB na kuwasukuma kufanya makubaliano mbalimbali ya ushirikiano, siri ya hilo ikiwa ni mazingira wezeshi yanayojengwa na serikali yake.

"Serikali ya Awamu ya Nane, NMB tuko katika kasi kubwa kusapoti jitihada hizo, ndio maana mwaka jana tumefungua matawi na vituo kadhaa, mwaka huu pia tutaongeza matawi matatu Zanzibar ya Nungwi, Wete na Mji Mkongwe ili kutanua wigo wa kuhudumia wazanzibar.

"Katika zao la mwani, tangu awamu hii ilipoonesha dira yake na tukavutiwa nayo, tukaanza kutoa elimu za fedha kwa wakulima wa mwani, wakulima wa chumvi, wavuvi na wajasiriamali wengine, ambako waliokidhi vigezo walikopesheka fedha na vitendea kazi.

"Kwahiyo, leo wizara yako inapokuja na ZASCO kwa lengo la kuongeza thamani ya zao hilo na ajira kwa ujumla, tukaona ni mkakati mzuri na kuamua kujitoa kuingia makubaliano haya kuwawezesha wakulima na kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla," alisisitiza Mponzi.

Aliongeza kuwa makubaliano hayo yanakwenda kuwezesha wakulima wa mwani wafanye kazi kwa ufanisi, kupata mazao kwa wingi na wanufaike punde watakapoyapeleka ZASCO kuongezwa thamani, jukumu lao kubwa likiwa ni kuwanoa wakulima bure na kuwapa elimu ya masuala ya fedha na biashara.

"Lingine, tutahakikisha kwamba tunawafikia wakulima wa mwani kote waliko, hata vijijini huko, tutawafikia tukiwa na masuluhisho yote ya kifedha, ambapo pia tutawafikishia huduma zetu zote zikiwamo wakala na huduma mpya sokoni hivi sasa ya NMB Pesa," alisema.

Alitoa rai kwa wazanzibar kuchangamkia huduma jumuishi za kifedha kupitia NMB Pesa, wafungue akaunti ili kuendelea kuunga mkono juhudi za benki hiyo ilizoonesha katika makubaliano mbalimbali waliyotia saini kwa nyakati tofauti.

Mponzi aliongeza: "Makubaliano hayo ni mkakati wa NMB katika si tu kuboresha huduma zake, bali pia kuongeza mchango wa sekta ya kilimo, huku ikisaidia kukuza uchumi hususani kwa hapa Zanzibar, mahali ambapo NMB tunajivunia kuwa sehemu ya ukuaji wa uchumi wa buluu."

Mkurugenzi Mkuu wa ZASCO, Dk. Masoud Mohammed Rashid, alishukuru NMB kuona umuhimu na haja ya kuungana na kampuni yake iliyoanzishwa kimkakati na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda katika kunyanyua zao la mwani, kwa kuwa makubaliano hayo yanakwenda kukipa thamani kilimo hicho.

"Makubaliano haya yamekuja wakati mwafaka kabisa, kwa sababu ZASCO imejenga kiwanda kikubwa zaidi Afrika, ambacho uwezo wake ni mkubwa sana kuchakata tani 30,000, lakini uzalishaji mwani Tanzania ni mdogo sana, tani 12,000, nguvu za ziada zinahitajika, ili kuongeza uzalishaji, ndio maana tunafurahishwa na ushirikiano huu na NMB," alisema.

# HABARI PICHA



Watumishi wa Kampuni ya Mafuta ya Puma Tanzania wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa hospitali ya wilaya ya Kigamboni huku wakiwa wameshika vifaa tiba ambavyo kampuni ya mafuta ya Puma Tanzania imekabidhi na kutumika katika wodi ya wanawake ya hospitali ya wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam. Puma wamekabidhi msaada huo leo Machi 8, 2024 wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake.



Menejimenti ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) katika picha ya pamoja na Watumishi Wanawake wa Mamlaka hiyo baada ya kuwakabidhi tuzo kwa kutambua hatua na juhudi walizofanya katika majukumu yao ndani ya TCAA. Mkurugenzi wa Udhibiti Uchumi TCAA Daniel Malanga (wa nne kutoka kushoto) aliongoza shughuli hiyo iliyofanyika wakati wa kuadhimisha siku ya kimataifa ya wanawake duniani jijini Dar es Salaam.




Mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani wilaya ya Muheza Ofisa Tarafa ya Ngomeni, Mohamed Katimba kushoto akipata maelezo kutoka kwa hakimu wa mahakama ya mwanzo Ngomeni, Bahati Manongi kulia alipotembelea banda la Mahakama katika Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika jana viwanja vya stendi ya Bombani. Kutoka kulia mhudumu wa mahakama ya mwanzo Mbaramo Sharifa Yasini na kushoto Hakimu wa Mahakama ya mwanzo, Mbaramo Thomas. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Katibu wa UWT Mkoa wa Tanga, Aziza Hussein Kiduba (kulia) akizungumza na madiwani wa viti maalum wilaya ya Muheza baada ya kukagua ujenzi wa nyumba mpya ya Katibu wa UWT wilaya hiyo eneo la Genge juzi ambapo kiongozi huyo alichangia saruji mifuko 15 na alizungumza na wanawake katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Wafanyakazi Wanawake wa mgodi wa Barrick North Mara wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kushiriki zoezi la kukabidhi msaada katika kituo cha kulea watoto cha City of Hope wilayani Tarime katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani mwishoni mwa wiki.

## Wabunge kupokea sura ya bajeti 24/25

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE leo wanatarajiwa kupokea sura ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2024/25, serikali itapowasilisha bungeni mapendekezo kuhusu mpango na kiwango cha ukomo wa bajeti kwa mwaka huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge jana, wabunge watapokea mapendekezo hayo kwa masharti ya Kanuni ya 116(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

Kanuni hiyo inasema 'tarehe kumi na moja ya mwezi Machi ya kila mwaka au tarehe ya siku nyingine ya kazi inayofuata iwapo tarehe hiyo itakuwa si siku ya kazi, waziri anayehusika na masuala ya mipango atawasilisha kwa wabunge, mapendekezo ya serikali ya mpango kwa mwaka wa fedha unaofuata'

Pia siku hiyo pia, waziri anayehusika na masuala ya fedha, atawasilisha kwa wabunge, mapendekezo ya serikali ya kiwango cha ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Baada ya mkutano huo, vikao vya kamati za kudumu za Bunge vitaanza kuanza Machi 11 hadi 30, mwaka huu kwa ajili ya mkutano wa Bunge la bajeti uliopangwa kuanza Aprili 2, mwaka huu.

Miongoni mwa shughuli za kamati ni kukagua utekelezaji miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/24 na kuchambua taarifa za utekelezaji bajeti kwa wizara zote.

Aidha, taarifa hiyo inaonesha kuwa kamati hizo za kisekta zitafanya ziara ya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, serikali kuu na taasisi za umma.

# Rais Kagame kuwania urais kwa mara ya nne

**KIGALI,** Rwanda

CHAMA tawala cha Rwanda, 'Rwandan Patriotic Front' (RPF), kimemteua Rais wa nchi hiyo Paul Kagame kuwa mgombea wake wa uchaguzi wa urais unaotarajiwa kufanyika Julai 15, mwaka huu kwa muhula wa nne wa miaka saba.

Inaelezwa kuwa RPF ilifanya maamuzi hayo juzi wakati wa kongamano baada ya kubaini kwamba Kagame hana upinzani.

Inaelezwa kuwa Rais Kagame mwenye umri wa miaka 66, ameitawala Rwanda tangu katikati ya miaka ya 1990 huku akishinda uchaguzi wa urais, kila mara kwa zaidi ya asilimia 90 ya kura, katika chaguzi za mwaka 2003, 2010 na 2017.

Aidha, inaelezwa kuwa mmoja wa washindani wake wachache katika uchaguzi wa urais ni kiongozi wa chama cha upinzani cha Green Party, Frank Habineza.

Inabainishwa kuwa mbunge mwenye umri wa miaka 47, alipata asilimia 0.45 pekee ya kura katika uchaguzi wa urais wa mwaka 2017 na kwamba anawekwa nafasi ya tatu kwa chaguzi za sasa, zinazokosolewa na vyama vya kutetea haki za binadamu kwa makosa yao na vitisho katika uchaguzi dhidi ya wapiga kura.



Pia inaelezwa kuwa mshindani mwingine wa Kagame, Victoire Ingabire, kiongozi wa vuguvugu ambalo halijasajiliwa la Dalfa Umurunzi likiwa na mada ya (Maendeleo na Uhuru kwa Wote), katika hatua hiyo ameondolewa kwenye kinyang'anyiro cha urais kutokana na kuhukumiwa hapo awali.

Hata hivyo, inabainishwa kuwa uamuzi wa mahakama uliopangwa kufanyika Machi 13 ndio utakaoamua iwapo ameidhinishwa kuwania urais au la.

Rwanda inapanga uchaguzi wake wa urais na wa wabunge Julai 15, kulingana na uamuzi wa mwaka jana wa serikali wa kufanya uchaguzi katika tarehe hiyo.

Wabunge 24 wanawake, wawakilishi wawili wa vijana na mwakilishi mmoja wa Wanyarwanda wenye ulemavu pia watachaguliwa na vyuo na kamati za uchaguzi Julai 16.

Kwa mujibu wa tume ya uchaguzi ya nchini humo wagombea watafanya kampeni kuanzia Juni 22 hadi Julai 12.

Rwanda inajionyesha kama moja ya nchi zilizo na utulivu katika bara la Afrika, lakini mashirika kadhaa ya haki za binadamu yanamshutumu Kagame kwa kuitawala katika mazingira ya hofu, kukandamiza upinzani na uhuru wa kujieleza. **RFI**



Hali ilivyo nchini Haiti baada ya waandamanaji kuibua machafuko. **PICHA MTANDAO**

# Msaada wa majini wabaki tegemeo Gaza

**GAZA,** Palestina

WANANCHI wa Ukanda wa Gaza wameelekeza matumaini yao kwenye misaada ya kwanza inayotarajiwa kuingia ukanda huo kwa njia ya

baharini, baada ya kubainishwa kuwa boti iliyobeba shehena ya tani 20 za mchele iko njiani ikitoka Cyprus kuelekea Gaza.

Inaelezwa kuwa boti hiyo inafanya safari hiyo muhimu katika wakati ambao Umoja wa Mataifa (UN) umetahadharisha juu ya kukaribia viwango vya juu vya baa la njaa kwenye Ukanda wa Gaza.

Tahadhari hiyo imetolewa katikati mwa mapigano yaliyoshika kasi kati ya vikosi vya Israel na wanamgambo wa kundi la Hamas, hali inayosababisha ugumu wa kuwasilishwa kwa misaada ya kibinadamu katika ukanda huo.

Meli ya hisani ya Marekani iitwayo, World Central Kitchen, imeshusha shehena ya misaada na kuipakia kwenye boti nyingine huko Cyprus tayari kwa safari ya kuelekea Gaza.

Inabainishwa kuwa shughuli hizo zinatumia bandari ya Larnaca na kwamba shehena za misaada zitafikishwa kaskazini mwa Gaza kupitia njia za maji baada ya nchi kavu kukumbwa na vikwazo kukuki.

Asasi ya Open Arms, mojawapo kati ya taasisi nyingi za hisani zinazoshiriki juhudi za kufikisha misaada ya kiutu kwenye Ukanda wa Gaza, inasema chombo chao kipo tayari kuanza safari watakapopewa ruhusa.

Ikibainisha kuwa njia ya bahari inalenga kukwepa vizuizi vya njia ya ardhini inaelezwa kuwa mpango wa kutumiwa njia ya bahari kufikisha misaada Gaza unaratibiwa kwa pamoja na Marekani, Umoja wa Ulaya (EU) na mataifa mengine washirika.

Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula Leyen aliyekuwa ziarani nchini Cyprus alisema kwamba msaada wa kwanza ungepelekwa Gaza jana kwa njia ya kutumia bahari kupitia Cyprus taifa la Umoja wa Ulaya lililo karibu zaidi na Ukanda wa

Gaza linalolenga kuepuka vikwazo vya kutumia njia ya ardhini, ambayo maofisa wa misaada ya kiutu na serikali za mataifa ya magharibi wameilaumu Israel kwamba inaiwekea vizingiti.

Inaelezwa kuwa kwa zaidi ya miezi mitano tangu kuzuka kwa vita wakazi milioni 2.4 wa Ukanda wa Gaza wanataabika kwa kukosa huduma muhimu husani wale wanaoishi upande wa kaskazini, eneo ambalo operesheni ya ardhini ya jeshi la Israel ilianzia.

Jitihada za hapo kabla za kutuma misaada ya ziada kwa njia ya anga hazijafua dafu na mashirika ya kimataifa yameendelea kutoa tahadhari kwamba umma wa Gaza unakabiliwa na hali mbaya.

Wizara ya Afya ya Ukanda wa Gaza inayoongozwa na kundi la Hamas, inasema watoto watatu zaidi wamepoteza maisha kutokana na utapiamlo na ukosefu wa maji mwilini.

Idadi hiyo inafanya jumla ya watoto waliokufa hadi sasa kwa sababu hizo kufikia 23.

Mapigano pia bado yanaendelea kwenye eneo hilo na hapo jana watu 82 waliuwawa kutokana na mashambulizi ya anga na ya ardhini ya majeshi ya Israel.

Kwa jumla wizara ya afya inasema hadi sasa watu 30,960 wengi wakiwa watoto na wanawake wameuawa tangu kuzuka kwa vita.

Vita hivyo, vilizuka mwisho mwa mwaka jana baada ya kundi la Hamas kufanya shambulizi kubwa ndani ya Israel mnamo Oktoba 7 na kusababisha vifo vya watu 1,200.

Licha ya jitihada za kutafuta makubaliano mapya ya kusitisha mapigano kati ya pande hizo mbili, hadi siku ya Jumamosi jioni dalili hazikuwa zimeonekana.

Rais Joe Biden ambaye aliahidi kwamba mkataba wa kusitishwa vita utapatikana siku za karibuni, alisema hadi sasa uwezekano wa hilo kutokea bado ni mgumu.

Kulikuwa na malengo ya kufanikisha usitishaji wa muda wa mapigano kabla ya mwezi mtukufu wa Ramadhan ulioanza leo. **DW**

# MSANII JAIVAH, WAFANYAKAZI NBC WACHANGIA SIKU YA WANAWAKE

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake duniani, msanii Jaivah, ambaye ni mmoja wa mabalozi wa Benki ya NBC na wafanyakazi wa benki hiyo wameungana na mamia ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kuchangia damu ili kuokoa maisha ya watu wenye uhitaji wa huduma hiyo muhimu.

Zoezi hilo la uchangiaji damu lilifanyika kwenye viunga vya makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kwa uratibu wa Umoja Wanawake wa benki hiyo, 'NBC Women Network Forum' ambao pamoja na zoezi hilo pia umoja huo umeratibu hafla fupi zilizohusisha wafanyakazi wa benki hiyo kwenye matawi yake mbalimbali nchini.

Benki hiyo pia ilitumia maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya 'Wekeza kwa Wanawake Kuharakisha Maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii' kugawa zawadi mbalimbali kwa wateja ikiwa ni mwendelezo wa kampeni yake ya 'NBC Buruda Time' inayopambwa na msaani Jaiva. Mbali na kukabidhi zawadi mbalimbali kwa wateja, msanii huyo pia alipata wasaa wa kuwaburudisha wafanyakazi na wateja wa benki hiyo.

**Akizungumza kwenye maadhimisho hayo Jaivah alitoa wito kwa jamii kuendelea kuchangia damu kwa wingi kwa kuwa inaokoa maisha ya watu wenye uhitaji. Alisisitiza umuhimu wa kila mtu kuchangia damu mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya hospitali yanafikiwa na kuokoa maisha ya watu wengi zaidi.**

''Kupitia Kampeni ya 'NBC Buruda Time', tumekuwa tukitoa zawadi na burudani kwa wateja wetu kama sehemu ya kushukuru kwa uaminifu wao. Kupitia maadhimisho tumeweza kutoa zawadi muhimu kuliko zote ambayo ni zawadi ya damu kwa wenzetu wenye uhitaji kwenye hospitali mbalimbali. Tunawahimiza wateja wetu waendelee kufurahia huduma bora za kibenki zinazotolewa na benki hii," alisisitiza Jaiva anayetamba na wimbo wake unaofahamika kama 'Buruda' akiwa ameshikirisha msanii Marioo.

Wakizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wenzao, Asha Mustafa na Johari Ntambwe, ambao pia ni viongozi waandamizi wa Umoja Wanawake wa NBC, walishukuru na kupongeza juhudi zinazofanywa na uongozi wa benki hiyo katika kusaidia wanawake wakiwamo wafanyakazi pamoja wajasiriamali katika kujikwamua kiuchumi na kuboresha maisha yao. Walisisitiza umuhimu wa kuwekeza kwa wanawake na kuhakikisha fursa sawa zinapatikana kwa kila mtu, bila kujali jinsia.

"Kwa ujumla, maadhimisho ya Siku ya Wanawake duniani yamekuwa ya mafanikio makubwa na yametupa fursa wafanyakazi wa Benki ya NBC na wadau wetu mbalimbali wakiwamo wateja kushirikiana katika kuchangia jambo muhimu la uchangiaji wa damu. Kupitia 'NBC Women Network Forum' tulijipanga kuhakikisha tunayatumia maadhimisho haya kuleta mabadiliko chanya katika jamii na kuendeleza maendeleo ya taifa letu, tunashukuru tumefanikiwa," alisema Ntambwe.



Balozi wa Kampeni ya 'NBC Buruda Time', inayoendeshwa na Benki ya NBC msanii Jaivah (kushoto), akichangia damu sambamba na wafanyakazi wa benki hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Zoezi hilo la uchangiaji damu lilifanyika kwenye viunga vya makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kwa uratibu wa Umoja Wanawake wa benki hiyo, 'NBC Women Network Forum'. **MPIGAPICHA WETU**

# *Viungo wawatesa mastraika ufungaji Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

VIUNGO washambuliaji wanaonekana kuwapelekesha mastraika kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara katika mbio za kuwania kinara wa ufungaji bora.

Hadi kufikia raundi ya 20 ya Ligi Kuu, viungo washambuliaji wanaonekana kuwa na uchu kwenye ufungaji wa mabao, wakiongozwa na Feisal Salum wa Azam FC pamoja na Stephane Aziz Ki wa Yanga.

Viungo washambuliaji ambao kazi yao mama ni kutoa pasi za mwisho kwa washambuliaji, badala yake wamegeuka kuwa wao ndiyo wafungaji wakiwafunika kwa kiasi kikubwa mastraika kwenye Ligi Kuu Bara.

Takwimu zinaonyesha kuwa Fei Toto anaongoza mpaka sasa kwenye orodha ya wafungaji, akiwa ameshapachika mabao 12, akifuatiwa na kiungo mshambuliaji mwenzake, Aziz Ki ambaye ametimiza mabao 11, wakiwa wanafukuzana.

Kama vile haitoshi, viungo washambuliaji wengine, Maxi Nzengeli wa Yanga na Marouf Tchakei wa Ihefu FC wanafuatia wakiwa na mabao manane kila mmoja.

Idadi hiyo ya mabao pia anayo straika Jean Baleke aliyekuwa akiichezea Simba, lakini mabao yake hayawezi tena kuongezeka kwa sababu hayupo tena kwenye Ligi Kuu Bara, na nafasi hiyo ameicha kwa straika mwenzake, Waziri Junior wa KMC.

Waziri ndiye straika mwenye mabao mengi mpaka sasa na anayeendelea kucheza ligi.

Kiungo mwingine, Mudathir Yahaya naye yumo kwenye mbio za kusaka Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Bara, akiwa wa moto, tayari amepachika mabao saba, sawa na mastraika Adam Adam wa Mashujaa FC, Samson Mbangula wa Prisons pamoja na Prince Dube wa Azam.

Hata hivyo, mbio za Dube kuelekea kutwaa kiatu hicho mbele ya viungo washambuliaji hao zinazonekana kugonga mwamba kwani amekuwa na mgogoro na klabu yake, akishinikiza kuondoka kwa sababu mbalimbali.

Kwa takwimu hizi inaonyesha huenda msimu huu mfungaji bora anaweza kuwa kiungo mshambuliaji, lakini pia kunaweza kukawa na idadi kubwa ya wanaomfuatia kuliko washambuliaji.

Msimu uliopita straika Fiston Mayele aliyekuwa akiichezea Yanga na kiungo mshambuliaji wa Simba walifungana wote wakiwa na mabao 17.

Mara ya mwisho kwa kiungo mshambuliaji kutwaa kiatu hicho peke yake ilikuwa ni 2017/18, ambapo kilikwenda kwa Emmanuel Okwi aliyekuwa akiichezea Simba aliyemaliza msimu huo wa Ligi Kuu Bara akiwa na mabao 20.

# Timu 12 zatinga 16-bora Kombe la FA Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya timu 12 zimefanikiwa kutinga hatua ya 16-bora ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, kwa Kanda ya Unguja.

Kutoka Ligi Kuu Zanzibar ni JKU SC, KMKM SC, Mafunzo SC, KVZ FC, Mlandege wakati Ligi Daraja la Kwanza ni Raskazone FC, Black Sailor FC, New King, Inter Zanzibar FC, Taifa Jang'ombe FC na Kilimani City na timu moja kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi ambayo ni Nyangobo FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ZFF, Ali Bakari 'Cheupe', alisema michezo ya mwisho ya kukamilisha hatua hii ya 32 bora ilitarajiwa kupigwa jana ili kupata timu nne zitakazoungana hizo 12 kuingia hatua ya 16-bora.

Alisema hatua hiyo ya 16 itaenedelea mwishoni mwa mwezi ujao kulingana na ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar itakayotolewa na Bodi ya Ligi baada ya kumaliza mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Aidha, Cheupe alizipongeza timu zote kwa kuonesha ushindani na mchezo wa kiungwani uwanjani katika hatua hiyo ya 32-bora.

Alisema timu zote zilicheza kwa ushindani mkubwa bila kuangalia madaraja wapinzani wao wanayotoka jambo lililoongeza ladha ya mashindano hayo, hivyo kufatiliwa na mashabiki wengi wa soka waliojitokeza viwanjani.

"Tunamaliza michezo minne ya hatua hii ya 32 ambapo tutapata timu nne zitakazoungana na hizi 12 kuingia hatua ya 16-bora, kikubwa nazipongeza klabu zote katika suala la kufuata kanuni ya mashindano, lakini pia katika kuonesha mchezo wa kiungwana uwanjani,"alisema.

Alisema kwa upande wa Kanda ya Pemba, michuano hiyo ipo katika hatua ya 16-bora na hatua ya nane bora itachezwa kama ilivyo kwa Kanda ya Unguja baada ya mwezi wa Ramadhani.

Hata hivyo, amewaomba wadau mbalimbali wa soka Zanzibar kujitokeza katika kudhamini michuano hiyo yenye ushindani mkali hasa kwa msimu huu.

Bingwa wa michuano hiyo atajinyakulia kitita cha Sh. milioni 30 kutoka kwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na ataiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**FODEN MKATABA MPYA**

KIUNGO wa kati wa England, Phil Foden, 23, anatazamiwa kuanza mazungumzo na Manchester City kuhusu mkataba mpya ambayo unaweza kumfanya kuwa miongoni mwa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

**NETO AWINDWA CITY**

MANCHESTER City ndio klabu ya hivi punde zaidi kuhusishwa na mshambuliaji wa Ureno, Pedro Neto, 23, ikiungana na Liverpool, Newcastle United na Arsenal katika kinyang'anyiro cha kumnasa winga huyo anayethaminishwa na Wolves kwa thamani ya angalau pauni milioni 60. ***(Telegraph)***

**UNITED KUSAJILI BEKI**

KLABU ya Manchester United inataka kuleta beki wa kushoto katika msimu ujao na wataunda orodha fupi mara tu muundo wao mpya wa bodi utakapokamilika. ***(Fabrizio Romano)***

**YORO PIA ATAKIWA**

MANCHESTER United pia inatumaini kumnunua beki wa kati wa Ufaransa, Leny Yoro, 18, kutoka Lille na inaweza kulipa pauni milioni 41 ili kukamilisha dili hilo. ***(Teamtalk)***

**WILLIAMS AFIKIRIWA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kushindana na Arsenal na Chelsea kumnunua mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Nico Williams, 21. ***(Mirror)***

**SPURS NA SON WAKE**

TOTTENHAM Hotspur ina imani kwamba mazungumzo ya mkataba mpya wa nahodha Son Heung-min, 31, yatafanikiwa. Mkataba wa sasa wa fowadi huyo wa Korea Kusini unatazamiwa kumalizika msimu wa majira ya joto 2025. ***(Give Me Sport)***

**GALLAGHER MAMBO BADO**

MAZUNGUMZO ya mkataba mpya kati ya kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, 24, na Chelsea yamekwama kwa sababu ya masuala ya kifedha katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

**PALHINHA ATAKIWA ARSENAL**

LIVERPOOOL na Arsenal wameongeza kasi yao ya kumnunua kiungo wa kati wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha, 28, lakini Bayern Munich, ambao walijaribu kumsajili mchezaji huyo msimu uliopita, bado wana nia naye. ***(Bild)***

**EDWARDS KUREJEA LIVER**

LIVERPOOL iko tayari kuthibitisha kurejea kwa Michael Edwards wiki ijayo, huku Richard Hughes akijiunga kama mkurugenzi wa michezo. ***(Sky Sports)***

**TONEY KUPUNGUZWA BEI**

KLABU ya Brentford itahitaji kupunguza gharama ya kumuuza mshambuliaji wa England, Ivan Toney, 27, ili kuendelea kuziweka Arsenal na Chelsea katika hali ya kutaka kumnunua mchezaji huyo. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS JR ANATENDEWA VIBAYA ZAIDI - ANCELOTTI

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema Vinicius Junior anatendewa vibaya zaidi uwanjani kuliko mchezaji yeyote ambaye amemfundisha katika maisha yake ya soka.

**Vinicius alifunga bao pekee la Madrid katika sare ya 1-1 ya raundi ya 16 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig kwenye Uwanja wa Bernabeu Jumatano, lakini pia alibahatika kutopata kadi ya njano kwa kumsukuma nahodha wa Leipzig, Willi Orban.**

Wikiendi iliyopita, fowadi huyo wa Brazil alipigiwa filimbi mara kwa mara na umati wa watu huko Mestalla wakati Madrid ilipotoka sare ya mabao 2-2 na Valencia - mchezo ambao pia alifunga mara mbili - baada ya kubaguliwa na kundi la mashabiki kwenye mechi hiyo hiyo msimu uliopita.

"Nimeangalia nyuma kidogo, katika historia, takwimu, na sijawahi kuona mchezaji ambaye aliteswa kama Vinicius," alisema Ancelotti katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana wa LaLiga wa Madrid dhidi ya Celta Vigo.

> ●●● Anapigwa teke, anapigiwa filimbi, anatukanwa na anafanya nini? Anafunga...

"Anapigwa teke, anapigiwa filimbi, anatukanwa. Na anafanya nini? Anafunga mabao na kutoa pasi za mabao. Halafu natakiwa kuzungumza naye kuhusu mtazamo wake? Hapana!

"Kila mtu anapaswa kubadili mtazamo wake kuhusu Vinicius. Katika historia yangu binafsi, mchezaji mwenye kipaji kikubwa hajawahi kuteseka na mambo ambayo Vinicius anayo. Huko Vallecas (dhidi ya Rayo Vallecano) alikatwa karate kichwani, na hakukuwa na hata kadi ya njano. Sasa kila mmoja anaomba kadi nyekundu kwa kusukuma dhidi ya Leipzig."

Vinicius amefunga mabao tisa katika mechi 18 za LaLiga msimu huu, na matatu katika mechi tano za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika kikosi cha Madrid, amezidiwa tu na Jude Bellingham, ambaye alikosa mechi ya Celta baada ya kufungiwa michezo miwili kwa kutolewa nje kwenye sare ya Valencia.

Bellingham alitolewa nje baada ya filimbi ya mwisho kwa kupinga uamuzi wa mwamuzi kumaliza mchezo sekunde chache kabla ya kupiga mpira wavuni kwa kichwa, kwa kile ambacho kingekuwa bao la ushindi.

"Tulikata rufaa kwa sababu tulifikiri adhabu ilikuwa nyingi," Ancelotti alisema. "Hakukuwa na matusi, ripoti ya mwamuzi ilisema hivyo. Kamati ya nidhamu ya RFEF ilitathmini njia ya fujo ambayo aliienda kwa mwamuzi.

"Natumai 'hawana 'namba yake'. Bellingham wakati mwingine hulalamika kama kila mtu, lakini wachezaji wengi hufanya hivyo kwa njia ya kutia chumvi kuliko Bellingham. Bado tunafikiri adhabu hiyo si sahihi."

HABARI MICHEZO




# ‘HAVERTZ ALITAKIWA APEWE UMEME’

**LONDON,** England

KOCHA wa Brentford, Thomas Frank, anaamini Kai Havertz alipaswa kupewa kadi nyekundu kabla ya kufunga bao la ushindi katika ushindi wa 2-1 wa Arsenal kwenye Uwanja wa Emirates Jumamosi.

Bao la kichwa la Havertz dakika ya 86 lilihitimisha mechi hiyo kali ambayo Declan Rice alifunga la kwanza kabla ya kipa wa Arsenal Aaron Ramsdale - kurudishiwa mpira langoni lakini akafanya makosa na wapinzani kusawazisha.

Ramsdale alianza katika mechi hiyo kutokana na David Raya kutostahili kucheza dhidi ya klabu yake kuu.

Havertz alioneshwa kadi ya njano kwa kumpiga kwa kiwiko Kristoffer Ajer kabla ya kugongana kidogo na Nathan Collins katika dakika ya 66, na hivyo kusababisha ukaguzi wa VAR kwa penalti.

Hakuna alichopewa na Havertz aliepuka kupata kadi kwani ni wazi alijidondosha kirahisi, jambo lililomkera Frank.

“Havertz alijiangusha na ni wazi na wazi,” alisema Frank.

“Natamani wangekubali tu, sijui kama anayo sababu hiyo hutokea kila mara, kila wiki kuna mtu anafanya, najua hutokea.

“Hiyo bila shaka ingelikuwa kadi ya pili ya njano na kadi nyekundu. Na kisha hangeweza kufunga bao la ushindi na tunatutumaini labda tungepata kasi zaidi, labda kushinda mchezo.”

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alisifu mchango wa Havertz baada ya mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 67.5 msimu wa majira ya joto kutoka Chelsea kuanza polepole kabla ya kufikia kiwango cha hali ya juu hivi karibuni, akifunga mabao manne na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi zake nne zilizopita za Ligi Kuu.

“Kama mtu angeniambia baada ya miezi miwili au mitatu ya kwanza kwamba uwanja mzima utaimba wimbo wake kwa mapenzi hayo, kwa hisia hizo, ingekuwa vigumu kuamini,” alisema Arteta.

“Hicho ndicho kinachotokea kwa watu wazuri. Ni mchezaji wa kipekee.”

# Rooney: Rashford anaweza kunipiku

**MANCHESTER,** England

WAYNE Rooney amesema anaamini Marcus Rashford ndiye mchezaji pekee katika klabu hiyo ambaye anaweza kumpita kama mfungaji bora wa muda wote wa Manchester United, lakini akasema anamhurumia kwa kuanza msimu kwa ugumu.

Rashford alifunga mabao 30 katika michuano yote msimu uliopita, lakini ameifungia United mabao saba pekee kwenye kampeni hii.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alipigwa faini na kuachwa nje ya ushindi wa United wa Kombe la FA raundi ya nne dhidi ya Newport County mwezi uliopita baada ya kujirusha kwenye klabu ya usiku ya Belfast wakati akidai kwamba alikuwa mgonjwa.

Akizungumza na TNT Sports Rooney alisema: “Rashford yupo katika nafasi ya upendeleo ambapo anachezea Manchester United.

“Nilishasema hapo awali, ndiye mchezaji mmoja ambaye niliamini kabisa angeweza kwenda kupata rekodi yangu ya ufungaji, na natumai atafanya hivyo kwa sababu ni kijana wa Manchester, lakini anahitaji kuwa na uthabiti.

“Kwa kweli, hana msimu bora zaidi, lakini anahitaji kupata kiwango na uthabiti na kuwa kiongozi wa timu hii.”

Rooney alifunga mabao 253 kwenye mechi 559 katika kipindi cha miaka 13 akiwa United, huku Rashford akiwa na nusu ya jumla ya mabao hayo.




# Kane hataki mchezo

**MUNICH,** Ujerumani

HARRY Kane alifunga hat-trick katika ushindi wa mabao 8-1 wa Bayern Munich dhidi ya Mainz Jumamosi na kuweka rekodi ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, huku mabingwa hao wakipunguza gepu la pointi kwa vinara Bayer Leverkusen hadi saba.

Kane, ambaye alijiunga msimu huu kwa rekodi ya ligi ya euro milioni 100 kutoka Tottenham Hotspur, amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga angalau mara mbili katika mechi nane tofauti katika msimu wake wa kwanza wa Bundesliga.

Pia alifikia rekodi ya Uwe Seeler ya kufunga mabao mengi katika kampeni ya kwanza ya Bundesliga kwa kufikisha jumla ya mabao 30.

Nahodha huyo wa England pia alifunga mabao mawili katika ushindi wa 3-0 Jumanne dhidi ya Lazio, ambao uliipeleka Bayern katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Bayern wana pointi 57 katika nafasi ya pili kwenye msimamo kabla ya mchezo wa nyumbani wa Leverkusen dhidi ya VfL Wolfsburg jana, Jumapili.



Kane alifungua akaunti yake dakika ya 13, na wakaongeza jingine kupitia kwa Leon Goretzka baada ya juhudi za Kane kutinga langoni dakika saba baadaye.

Mainz walisawazisha kwa muda mfupi kwa mkwaju wa faulo wa Nadiem Amiri na wageni wakasukuma kwa nguvu kutafuta bao la pili kabla ya Kane kurejesha utulivu katika muda wa dakika za lala salama.

Wenyeji waliishinda Mainz tangu mwanzo wa kipindi cha pili na Thomas Mueller akakamilisha hatua ya haraka na kufanya mambo kuwa 4-1 katika dakika ya 47.

Huku safu ya ulinzi ya Mainz ikiwa imevurugika kabisa, wenyeji waliendelea kumiminika na Jamal Musiala akafumua shuti lililopita wavuni kabla ya mchezaji wa akiba Serge Gnabry kugeuza kisigino cha katikati ya angani kufanya matokeo kuwa 6-1.

Kane alikamilisha hat-trick yake akiwa karibu na goli, akiunganisha kwa kichwa mpira uliorudiwa kwenye lango la mbali na mpira wa kichwa wa Goretzka dakika za lala salama ukakamilisha ushindi huo.

# Azam FC waanza kuiwinda Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, ameanza kuzinoa silaha zake kuhakikisha wanafanikiwa kupata ushindi katika mchezo wao unaofuata dhidi ya Yanga.

Amesema anasahihisha makosa yao kwenye safu ya ulinzi na ushambuliaji ili kuwa makini katika mchezo ujao watakaocheza na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

Akizungumza na Nipashe jana, Dabo alisema baada ya kutoka sare ya bao 1-1 na Coastal Union, wamerejea katika uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kusahihisha baadhi ya makosa yao.

Alisema sehemu zote zilikuwa na makosa, safu ya ulinzi na ushambuliaji, ameelekeza umakini wake katika maeneo hayo kwa sababu mechi inayofuata wanazitaka pointi tatu kwa kutowapa wapinzani nafasi ya kufanya mashambulizi.

"Washambuliaji nao wanatakiwa kuwa makini hasa nafasi tunazotengeneza, tunapoteza nafasi nyingi, katika hilo tunafanyia kazi kujiandaa na mchezo wetu unaofuata dhidi ya Yanga," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa, wanachoangalia zaidi ni kutafuta pointi katika kila mchezo uliopo mbele yao ili kufikia malengo yao pamoja na mashabiki kuona timu yao inacheza mpira mzuri na kupata matokeo mazuri.

Jumapili wiki hii, Azam FC watakuwa nyumbani katika mchezo wa mzunguko wa pili wa ligi hiyo ikiwakaribisha Yanga, kwenye dimba la Azam Complex lililopo Chamazi jijini Dar es Salaam.

# TUZO ZA WANAWAKE KATIKA UONGOZI AFRIKA, 25 WATUZWA

**Na Mwandiahi Wetu**

TUZO za Wanawake Katika Uongozi Afrika zimesherehekea hatua muhimu ya kutimiza miaka mitano kwa kuwatambua viongozi 25 wa kipekee wa kike kutoka kote barani humu.

Hafla hiyo ya kifahari ya chakula cha jioni ilifanyika katika Hoteli ya Hyatt Regency Kilimanjaro jijini Dar es Salaam juzi, ikiongozwa na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, pia ilipewa heshima kwa uwepo wa Tri Yogo Jatmiko, Balozi wa Indonesia nchini Tanzania, pamoja na waheshimiwa wadau wengine na vinara kutoka sekta mbalimbali.

Akizingumza kwenye halfa hiyo, Naibu Waziri Mwanaidi, aliipongeza taasisi hiyo kwa juhudi zake za kulea mitandao inayowasaidia wanawake katika safari zao za uongozi.

Alisema tuzo hizo zimesalia kuwa thabiti katika dhamira yake ya kutambua na kusherehekea mafanikio ya viongozi wa kike ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika nyanja na jumuiya zao.

**Naibu Waziri huyo, alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, tuzo hizo zimetumika kama kinara cha kutia moyo, kukuza uwezeshaji na kutetea tofauti za kijinsia na ushirikishwaji kote Afrika.**

Naye Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Wanawake katika Uongozi Afrika (Women In Management Africa), Dk. Naike Moshi, alisisitiza kujitolea kwa shirika hilo katika kuimarisha usawa wa kijinsia na utofauti wa kijinsia kwenye bodi na majukumu ya uongozi, kwa kuzingatia vigezo vya kimataifa vya mazoea endelevu ya biashara na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

"Leo, tunasherehekea mafanikio makubwa ya viongozi wanawake, hasa tukiangazia nafasi ya urais wa Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan wa Tanzania. Kupaa kwa Dk. Hassan kwenye kiti cha urais kunaashiria hatua ya kihistoria, kwani amekua rais wa kwanza mwanamke nchini, na kuwatia moyo watu wengi kwa kujitolea kwake bila kuyumba katika utumishi wa umma na utetezi wa ushirikishwaji wa wanawake katika michakato ya maamuzi.

"Uongozi wake unasisitiza uwezo mkubwa wa wanawake katika nyadhifa za madaraka, ukiwa mfano mzuri kwa vizazi vijavyo. Pia tunatambua michango ya kudumu ya wanawake katika historia na tunathibitisha tena dhamira yetu ya kuendeleza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake duniani kote," alisema Naike.

Washindi 25 bora waliotunukiwa katika hafla ya mwaka huu ya Wanawake Katika Uongozi Afrika ni; Anagha Bhattbhatt (Tanzania), Brenda Deborah Shuma (Tanzania), Carlotta Dal Lago (Kenya), Caroline Mohoni (Tanzania), Doreen Mangesho (Tanzania), Dk. Tia Murry (Marekani), Dk. Aisa Muya (Tanzania), Ebonie Mbeteni (Tanzania) na Mwandisi Fatuma Mwamba (Tanzania).

Wengine Gloria Kahamba, Grace Gathuri, Ilona Felten, Jamila AL Nofly (wote kutoka Tanzania), Mamela Luthuli wa Africa Kusini, Naomi Serbantez (Tanzania), Penny Mkhize (Afrika Kusini), Prof. Linda Mhando (Marekani), Rahma Abdullahtif Musoke (Tanzania).

Katika orodha hiyo pia wamo Reanne Olivier (Marekani), Rewa Udoji (Nigeria), Rita Moses Mbeba (Tanzania), Sarah Kabil (Misri), Siza Mkoma (Tanzania), Stella Keshubi (Uganda) na Tumaini Kivuyo (Tanzania).



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis (katikati) katika picha ya pamoja na washindi wa Tuzo ya Wanawake Katika Uongozi Afrika wakiwa na tuzo zao ya kutunukiwa mwishoni mwa wiki. Kushoto kwake ni Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Wanawake Katika Uongozi Afrika (Women In Management Africa), Dk. Naike Moshi. **MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Simba akataa kutupa...

INATOKA UKURASA 24

Alisema bado wana tatizo la kutumia nafasi wanazozipata, lakini wanashindwa kurekebisha kwa sababu ya kukosa muda.

"Ni kweli bado tuna tatizo la kutotumia nafasi, tumekuwa tukitengeneza nafasi nyingi, lakini tunashindwa kuzitumia, hii inasababishwa na kwamba kwa sasa tunakosa muda wa kusahihisha makosa kwenye viwanja vya mazoezi kwa kuwa kila baada ya siku mbili tunacheza mechi, lakini yote kwa yote tutarudi mazoezini na kuyafanyia kazi ili nafasi tunazozipata tuzitengeneze kuwa mabao."

Kocha huyo pia ameonekana kufurahia kurejea Azam Complex, kwani kuna faida nyingi kwao kuliko hasara na hasa kiufundi.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, David Ouma, amewapongeza Simba kwa ushindi akisema timu yake ilistahili kupoteza, hasa baada ya kukosa mabao kadhaa kabla ya wapinzani wao kupata bao la pili.

"Nafikiri ni mechi ambayo tulistahili kupoteza, nawapongeza Simba kwa kushinda mchezo huu."

Willy Onana, alifunga bao la ushindi, ambapo kabla ya hapo, Freddy Michael alikuwa ameipatia Simba bao, Lucas Kikoti akisawazisha.

# *Gamondi ataja ugumu wa Ihefu*

INATOKA UKURASA 24

"Kitu muhimu kwangu ni kutumia nafasi vizuri na kucheza mpira mzuri ambao tutafanikiwa malengo yetu, kila siku naomba Wananchi waje uwanjani, wasahau matokeo ya mechi iliyopita waje kwa wingi kuisapoti timu yao na kuona kiwango kizuri," alisema Gamondi.

Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Mecky Maxime, alisema mechi hiyo si rahisi kwa kuwa Yanga ni bora wanaongoza ligi na wamefanya mazoezi kulingana na ubora na madhaifu ya wapinzani wao, ila kikubwa kwao wanahitaji pointi tatu.

"Kikubwa tunaingia kwa tahadhari kucheza kwa nidhamu kubwa na kuangalia ni muda gani wa kushambulia na kuzuia, kazi yangu ni kutengeneza vijana na kuwapa njia ya kuweza kupata matokeo mazuri.

"Tunekuwa tukipata nafasi nyingi na tunazitumia chache, lakini mechi ya kesho (leo), itakuwa nzuri kwa sababu tunahitaji kupata matokeo, tuna timu nzuri na tunahitaji pointi tatu hakuna kingine, " alisema Maxime.

Mwakilishi wa wachezaji wa Ihefu FC, Fikirini Bakari alisema wako tayari kwa mchezo wa leo na wataingia kwa tahadhari kubwa kwa sababu wanatambua ukubwa wa Yanga.

"Tumejipanga vizuri na tutacheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu tumefanikuwa kuwaona wapinzani wetu, Yanga wanavyocheza na benchi la ufundi tayari limemaliza majukumu yao kazi kubwa ni kwetu kutafuta pointi muhimu katika mchezo wetu wa leo," alisema Fikirini.

Michezo
Jumatatu Machi 11, 2024
Nipashe




‘Havertz alitakiwa kupewa umeme’ UKURASA 22



Mecky Maxime

Miguel Gamondi

# Gamondi ataja ugumu wa Ihefu Chamazi leo

**Na Saada Akida**

## ●●● Mexime asema ni mechi ngumu lakini wanataka matokeo, wamejipanga...

WAKATI vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wakishuka dimbani leo kusaka pointi tatu muhimu mbele ya Ihefu FC katika mchezo wa mzunguko wa pili wa ligi hiyo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, ameeleza sababu ya mchezo huo kuwa ugumu, lakini akasema “tunazitaka pointi tatu”.

Mchezo huo utakapigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, majira ya saa 1:00 usiku ambapo timu zote zinahitaji pointi tatu, huku Yanga ikihitaji kulipa kisasi baada ya duru la kwanza kupoteza pointi zote tatu ugenini.

Katika mchezo wa duru la kwanza Oktoba 4, mwaka jana, Yanga walikubali kichapo cha mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbalali mkoni Mbeya.

**Ihefu FC ni timu pekee msimi huu imefanikiwa kuifunga Yanga ambao kipigo hicho bado kipo katika kumbukumbu zao na leo wanakutana katika mzunguko wa pili na wakitaka kuendeleza walipoishia huku wenyeji wao wakitaka kulipa kisasi.**

Kwa misimu mitatu timu hizo zilipokutana Ihefu FC imepoteza mechi tatu, imeshinda mbili na sare moja, hivyo mchezo wa leo kila moja imedhamiria kusaka pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kuelekea mchezo huo, Kocha wa Yanga, Gamondi amesema wametoka kucheza mechi Ijumaa iliyopita na wamerejea na kupata siku moja ya kujiweka sawa kwa ajili mchezo huo wa leo.

Alisema ataendelea kuwakosa baadhi ya wachezaji sita waliokosekana mechi iliyopita akiwamo Khalid Aucho ambaye anefanyiwa upasuaji mdogo wa goti.

“Wachezaji wako tayari kwa ajili ya kuwakabili Ihefu FC, itakuwa mechi ngumu na ushindani kwa sababu tunakutana na timu bora tofauti ya tuliyokutana nayo katika mzunguko wa kwanza, (hii ni kwa sababu) wamefanya maboresho kuanzia benchi la ufundi na kuongeza baadhi ya wachezaji wazuri.

INAENDELEA UKURASA 23

# Kocha Simba akataa kutupa taulo ubingwa

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amekataa kutupa ‘taulo’ kwa watani wao wa jadi, Yanga, akisema mechi bado zipo nyingi ambazo zinaweza kuwapatia ubingwa wa Tanzania Bara, huku akikiri kuna tatizo la wachezaji wake kushindwa kutumia nafasi nyingi wanazotengeneza.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga juzi baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union, Matola alisema pamoja na kwamba Yanga inaendelea kufanya vema, lakini wao hawajakata tamaa kwa sababu ligi ni kama mbio ndefu, anayechanga karata zake vizuri mwishoni mwa kumalizika ndiyo mshindi na si yule anayeongoza kwa muda mrefu.

“Siwezi kusema eti ubingwa basi kwa sababu kuna timu inafanya vizuri, sisi bado tupo kwenye mbio hizo na tuna imani tunaweza kuupata, siku zote ligi ni kama mbio ndefu, mwanariadha anaweza kuongoza kwa muda mrefu, akawa mbele kilometa nyingi, lakini zikibaki mita kadhaa watu wanapindua kibao, hii ni raundi ya 20, lakini sisi Simba tumecheza mechi 17, hivyo michezo mingi imebaki , huwezi kututoa kwenye ubingwa,” alisema Matola.

Akiuzungumzia mchezo huo alisema ulikuwa mgumu kwa sababu nyingi, moja ni kwamba siku zote hata wakati wao wanacheza, wakikutana na Coastal Union mechi inakuwa ngumu mno, lakini kingine ni uchovu wa wachezaji.

“Niwapongeze wachezaji wetu wamepambana na kutupatia pointi tatu ambazo kwa leo tulizihitaji kuliko kitu kingine chochote.

“Siku zote mechi za Simba na Coastal tangu sisi tunacheza zinakuwa ni ngumu, ingawa huwa tunawafunga mara kwa mara, kilichotupa ugumu mwingine ni kwamba tunacheza mechi mfululizo, wachezaji wanapata uchovu wa mwili, hii ilisababisha mechi ya leo kwetu iwe ngumu,” alisema Matola.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >